


# Hadithi za Kiunguja

## Short Stories as Related by Natives of Zanzibar

Compiled & Edited by

Edward Steere

1867

# HADITHI ZA KIUNGUJA.

## SHORT STORIES

AS RELATED BY NATIVES OF

ZANZIBAR.

SO
LI
DEO
GL
OR
IA

ZANZIBAR.

1867.

PRINTED AT THE CENTRAL AFRICAN MISSION PRESS,
ZANZIBAR.

## CONTENTS.


Kisa cha Mwewe na Kunguru . . p. 1
Sungura na Simba . . . . . . . „ 3
Pepo aliyedanganywa na mtoto wa Sultani „ 7
Vitendawili . . . . . . . . . „ 13
Ao rathi, ao mali . . . . . . . „ 14
Kisa cha Hassibu Karim ad Din na Sultani wa nyoka . . . . . . . „ 25
Mtu ayari na hamali . . . . . . „ 44
Utumbuizo wa Gungu . . . . . . „ 45
Hadithi ya Liongo . . . . . . . „ 49
Mifano . . . . . . . . . . „ 56
Uza ghali si uza rakhisi . . . . . „ 57


APPENDIX.


A translation of the Verses at pp. 15 - 8 into the current language of Zanzibar.

# CORRIGENDA.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| P. 2 | l. 3 | *for* | mwenzangu | *read* | wenzangu |
| „ 4 | „ 7 | „ | nakjua | .. | 'nnakuja |
| „ 5 | „ 8 | „ | uningoja | „ | uningoje |
| „ 12 | „ 4 | „ | aka'mpeleka | „ | aka'mpelekea |
| „ 15 | „ 19 | „ | aka'mka | „ | akaa'mka |
| „ 19 | „ 13 | „ | ukapikiwa | „ | akapikiwa |
| | | „ | ukapelekewa | „ | akapelekewa |
| „ 22 | „ 6 | „ | akafnrahi | „ | akafurahi |
| „ 23 | „ 7 | „ | akawaga | „ | akawaaga |
| „ 24 | „ 18 | „ | akadnda | „ | akaenda |
| „ 40 | „ 24 | „ | niki'fuata | „ | niki'mfuata |
| „ 55 | „ 23 | „ | wakamwona | „ | kamwona |
| „ 68 | „ 1 | „ | mweyi | „ | mwenyi |
| | 10 | „ | Snltani | „ | Sultani |

Pp. 69 & 70 *are erroneously numbered* 67 & 68

P.71 l.16 *for* mcbunga *read* mchunga

## KISA CHA MWEWE NA KUNGURU.

ALIONDOKA Sultani ya kunguru, aka'mpelekea waraka Sultani ya mwewe, akamwambia, nataka uwe asikari yangu. Akamwambia sikubali. Akamwambia, kama hukubali tutapigana, mimi nawe. Akamwambia, na tupigane, ukinishinda nitakufuata, nikikushinda weye utanifuata.

Wakapigana, kunguru wakashindwa. Akaondoka mzee 'mmoja, akawaambia — tukimbie. Wakakimbia katika 'mji wao, wakaenenda 'mji mgine. Mwewe walipokuja wasimwone mtu, wakakaa katika 'mji wa kunguru.

Hatta siku nyingi kunguru wakafanya shauri. Akaondoka mzee, akasema, ninyonyoeni manyoya mukanitupe mjini wa mwewe. Waka'mnyonyoa, wakaenda, waka'mtupa.

Walipopita mwewe, wakamwona, wakamwambia, wafanya nini huku mjini kwetu? Akawaambia, wenzangu wamenipiga wamenitoa 'mji kwa sababu nimewaambia, 'mfuateni mwewe.

Wale waka'mchukua, wakaenda naye kwa

Sultani yao, wakamwambia, huyu kunguru tumemwokota, naye mwulize, atasema maneno yake.

Sultani akamwuliza, akamwambia, mwenzangu wamenipiga, wamenitoa 'mji kwa sababu naliwaambia kweli 'mfuateni mwewe, ndio Sultani, wakanipiga. Sultani ya mwewe akamwambia, kaa kitako hapa.

Akakaa kitako siku nyingi. Hatta siku moja wakaenda kanisani, nayee waka'mchukua, wakasali pamoja, hatta walipotoka, wakamwuliza, sisi na ninyi, nani anaabudu sana Muungu? Akawaambia, ninyi.

Akakaa kitako waka'mpenda sana. Hatta siku kuu yao ikikaribia, akatoka usiku, akaenda, akawaambia wenziwe, kesho watakwenda kanisani wote, njooni nje ya mlango wa kanisa, mutie moto. Wale wakatoka, wakaenda ku tafuta kuni na wangine wakachukua moto.

Hatta assubui wakaenda zao kanisani, asisalie mtu katika 'mji, ela yule mzee kunguru. Wakamwambia, kwa nini huenendi kanisani leo? Akawaambia, tumbo linaniuma sana. Wakamwambia, bass. Akaenda, akawaita wenziwe. Akawaambia, wamekwisha ku ingia kanisani wote.

Wakaenda wale, wakatia kuni katika mlango

wa kanisa, na wangine wakatia moto. Moto ukawaka. Wakaona moshi waingia ndani ya kanisa, wakakimbia madirishani, na wangine wakafa wengi sana na Sultani pia akafa. Kunguru wakatwaa 'mji.

Wale waliobaki mwewe wakawakimbia kunguru hatta leo.

## SUNGURA NA SIMBA.

ALIONDOKA Sungura ku enda ku tafuta chakula mwituni, akaona mbuyu mkubwa sana, akatazama ju, akaona mzinga wa asali ya nyuki. Akarudi mjini ku enda ku tafuta wenziwe wakuja kula naye.

Akapita mlangoni kwa Buku, aka'mkaribisha buku wakakaa kitako. Akamwambia, baba yangu amekufa, ameniachia mzinga moja wa asali, bassi twende tukale. Wakaenda.

Akamwambia, panda ju. Wakapanda wote wawili. wakala asali Nao wamechukua mienge ya moto, wakachoma nyuki, wakachimbia. Wakazima moto, wakala asali.

Marra akatoka Simba chini ya mbuyu. Akatazama ju, akaona watu wanakula, akawauliza—

Nani ninyi? Sungura akamwambia buku, nyamaza, ana wazimo mzee yule. Akawauliza tena Nani ninyi, ha'msemi? Buku akaogopa, akamwambia, sisi hapa.

Sungura akamwambia buku. Nitwae mimi, unitie ndani ya mwenge, umwambie mzee simba, jitenge nitupe mwenge, nami nakjua. Simba akajitenga, akatupa buku, ukianguka chini sungura akatoka akakimbia.

Simba akamwambia, shuka bassi. Akashuka. Aka'mkamata, akamwambia, walikuwa weye na nani uko ju? Akamwambia, mimi na sungura. Hukumwona hapa nilipo'mtupa? Akamwambia, sikumwona. Aka'mla buku. Simba akatoka ku enda ku 'mtafuta sungura, asimwone.

Hatta siku ya tatu sungura akaenda, akamwita kobe, akamwambia, twende, tukale asali. Akamwuliza — ya nani? Akamwambia, ya baba yangu. Akamwambia, twende. Wakafika, wakapanda ju na mienge yao ya moto, wakachoma nyuki, wakakimbia, wakakaa kitako, wakala.

Marra akatokea simba, na yule simba ndio mwenyewe asali. Akawauliza, nani ninyi ju? Sungura akamwambia kobe, nyamaza. Akauliza tena simba. Kobe akaogopa, akamwambia, mimi nitasema, umeniambia asali hii yako, kumbe

si yako, ya mwenyewe simba? Simba akauliza tena, nani ninyi? Akamwambia, sisi hapa. Akawaambia, shukeni bass. Akamwambia, tunakuja. Na simba aka'mtafuta sungura siku nyingi, akasema, leo nitapata sungura.

Sungura akamwambia kobe, unitwae mimi unitie ndani ya mwenge, umwambie simba, jitenge nitupe mwenge, nami nitakwenda, uningoja chini. Akamwambia — Vema. Kobe akasema moyoni mwake, huyu ataka ku kimbia ku niacha mimi niliwe na simba, ataliwa yee mbele. Aka'mtwaa aka'mtia ndani ya mwenge. Akamwambia simba. Sungura huyu anakuja.

Simba akamdaka, aka'mkamata mkononi, akamwambia, nikufanyeje leo? Akamwambia, ukinila nyama yangu ngumu. Simba akamwuliza, nikufanyeje bassi? Akamwambia, nikamata mkia unizungushe, kiisha unipige na inchi, bassi utanila. Simba akahadaika, aka'mzungusha, akitaka ku 'mpiga, akachopoka mkononi, akaenda mbio. Aka'mkosa sungura.

Akamwambia kobe, shuka na weye. Akashuka. Akamwambia, nikufanyeje nawe? Akamwambia nitia katika tope, unisugue hivi, hatta nibanduke maganda. Aka'mchukua simba, akaenda naye majini aka'msugua, kobe akakimbia, si-

mba akasugua mikono hatta ikachubuka. Akaangalia mikono yake inatoka damu, akanena, amenitenda leo sungura. Akaenda ku 'mtafuta.

Akauliza, nyumba ya sungura iwapi? Wakamwambia, hatuijui. Na sungura amemwambia mkewe, tuhame nyumba hii. Wakahama. Simba akenda ku uliza tena, wakamwambia watu, nyumba yake ile ju ya mlima. Akaenda simba, hatta akifika, hako sungura. Akasema, nitajificha ndani ya nyumba, hatta sungura akija na mkewe, nitawala wote wawili.

Akaja sungura, yee na mkewe, hana habari, hatta njiani akaona miguu ya simba, akamwambia mkewe, rudi weye, simba amepita hapa ananitafuta mimi. Akamwambia, sirudi, nitakufwata mume wangu. Akamwambia, weye mtoto wa watu, rudi. Akarudi. Sungura akaenenda, akafwata miguu, akaona imeingia ndani ya nyumba yake. Akasema — Loo! simba umo ndani.

Akarudi taratibu, akaenda akasimama mbali, akatoa salaamu, akasema — Salaam nyumba! Salaam nyumba! Salaamu nyumba! Akasikia kimya. Akanena sungura, gissi gani killa siku nikipita hapa, nikitoa salaamu, nyumba hunijibu, labuda leo 'mna mtu umo ndani. Yule simba akadanganika, akatikia — Salaamu!

Akamwambia — Looo! simba umo ndani, wataka ku nila mimi mwanayo, ukasikia wapi nyumba ku sema? Simba akamwambia, uningoje bass. Sungura akakimbia, wakafukuzana hatta simba akachoka. Akawaambia watu, sungura akanishinda, bass, si'mtaki tena. Akarudi.

## PEPO ALIYEDANGANYWA NA MTOTO WA SULTANI.

PALIKUWANA Sultani akitamani kijana siku nyingi, asipate. Naye ana mali mengi na miji mingi. Akaona — nikifa, itapotea mulki huu pia kwa sababu ya ku kosa mtoto.

Akaja sheitani akajifanya kama mtu, akamwambia Sultani, nikikupa dawa, ukipata mtoto, utanipa nini? Akamwambia, nitakupa nussu ya mali yangu. Akamwambia, sitakubali. Akamwambia, nitakupa miji yangu nussu. Akamwambia, sikubali. Akamwambia, wataka nini bass? Akamwambia, ukizaa watoto wawili, nipe 'mmoja, nawe utwae 'mmoja. Akamwambia, nimekubali.

Aka'mletea dawa, akamwambia, 'mpe mkewo, ale. Aka'mpa, akala. akachukua mimba, akazaa mtoto wa kwanza manamume, na wa pili manamume, na wa tatu tena manamume.

Akaja rafiki yake yule alio'mpa dawa, akamwambia — haya, tugawanye. Akamwambia, bado, hawajasoma watoto hawa. Akamwambia, nipe mimi nikawasomeshe, akamwambia, chukua. Akenda nayo kwake. Na nyumba kubwa kwake, na killa kitu kimo ndani.

Akawasomesha hatta wakajua elimu pia, wakafanya harufi, akaisha akawapelekea baba yao. Na wale vijana 'mmoja hodari sana. Akamwambia babayo, njoo, tugawanye watoto leo, akamwambia, gawa weye. Akagawanya yee, akatwaa wawili akaweka mbali, akatwaa na 'mmoja, aka'mweka mbali, akamwambia — Chagua Sultani! Sultani akatwaa wale wawili, na yule akatwaa 'mmoja, akaenda zake.

Akaenda kwake, aka'mpa funguo zote, akamwambia, killa utakacho fungua. Yule kijana akakaa kitako ndani ya nyumba, na yule babaye ku toka akaenda ku tembea mwezi, hatta anaporudi.

Bass, kijana akakaa kitako, hatta siku moja, akachukua ufunguo, AKAendA, AKAfunguA chu-

mba kimoja. Akaona thahabu kana maji, akatia kidole ikashika, akaisha ku futa haitoki, akafunga kitambaa. Akaja baba yake, akamwuliza, una nini kidole? Akamwambia, nimejikata. Akakaa hatta siku ya pili, baba yake akatoka, akaenda zake ku tembea.

Yule mtoto akachukua funguo zote, akaenda ku fungua chumba cha kwanza, akaona mifupa ya mbuzi, akafungua cha pili, akaona mifupa ya kondoo, akafungua cha tatu, akaona ya ngombe, akafungua cha 'nne, akaona ya punda, akafungua cha tanu, akaona ya farasi, akafungua cha sita, akaona vitwa vya watu, akafungua cha saba, akaona farasi mzima.

Akamwambia, ewe binadamu! watoka wapi? Akamwambia, mimi, babayangu huyu. Akamwambia, kazi yake kula watu, na punda, na farasi, na ngombe, na buzi, na killa kitu, na sasa tumesalia mimi nawe.

Akamwambia, tufanyeje? Akamwambia, njoo unifungue, aka'mfungua. Akamwambia, sasa fungua chumba cha mali, mimi nitameza killa kitu, na baba yako akija akaenda ku waita watu kuja ku tula, na akija, atakwambia, twendee kuni, useme mimi sijui kazi hiyo, atakwenda yeye pekeyake, akija nazo atateleka sufuria kubwa, atakwambia,

chochea moto, mwambia, siwezi, atakwenda mwenyewe ku chochea moto, ataleta sa'mli nyingi, ataitia ndani ya sufuria, hatta ikipata moto atafunga p'embea, atakwambia, panda ucheze, mwambia, sijui mimi ku cheza mchezo huu panda wewe mwenyewe nikuangalie kwanza na mimi nipate ku fanyiza kana weye, akipanda yeye ku kuonyesha, 'msukume ndani ya sufuria ya sa'mli ya moto, uje zako mbio, na miye nitakwenda ku kungoja chini ya mti uko njiani.

Farasi akakimbia, akamwacha 'mtoto pekeyake. Hatta alipokuja baba yake, akamwambia, kesho twendee kuni. Akamwambia, mimi sijui kazi hiyo. Akamwambia, bass, kaa kitako. Akaenda mwenyewe pekeyake, akaleta kuni nyingi. Naye amekwisha waambia watu, kesho na karamu, njooni. Akaja akatoa sufuria akateleka, akamwambia, tia kuni, akamwambia, sijui mimi. Akamwambia, kaleta sa'mli, akamwambia, siwezi kuichukua, sina nguvu. Akaenda mwenyewe, akaichukua, akaitia ndani ya sufuria, akatia moto. Akamwambia, chochea, akamwambia, sijui ku chochea moto.

Akamwambia, umewona mchezo wa kwetu? Akamwambia, sijauona bado. Na sa'mli imepata moto sana. Akafunga p'embea, akamwambia,

panda hapa, nikuonyeshe. Akamwambia, panda mwenyewe kwanza, ucheze, nami nikiona baba, nipate ku cheza. Akapanda, akacheza. Akashika, aka'msukuma ndani ya sufuria, akatokota pamoja na sa'mli, akafa.

Akakimbia mtoto, akaenda hatta chini ya mti akaona farasi akaja mbio. Farasi akaja, aka'mkamata, aka'mweka ju ya maungo yake, akamwambia, twende zetu sasa. Wakaenda zao.

Wale wenziwe kule wakaja, waka'mtafuta, hawamwoni. Na njaa inawauma sana, wakaangalia ndani ya sufuria wakaona chakula kimekwisha, wakasema, katule chakula hiki, wakaipua wakapakua, wakala. Hatta walipokwisha, waka'mtafuta, hawamwoni. Wakaingia ndani ya nyumba, wakatoa vyakula pia na michele pia, wakaja wakapika, wakala, siku ya pili tena, wakaona hajaja, wakaenda zao kwao.

Huyu mtoto, yee na farasi wakaenda hatta mbali miji mingine, wakakaa mwisho wa mji. Akamwambia hapa tukae, wakakaa, wakala chakula. Akamwambia. hapa tujenge nyumba, wakajenga nyumba kubwa na killa kitu ndani, wakatia punda na farasi na ngombe na buzi na watumwa, wakakaa.

Hatta siku yule Sultani akasikia, akaenda, a-

kapeleka watu, wakaenda ku tezama kweli habari iko nyumba kubwa, watu waambia, kweli Sultani, ni nyumba kubwa.

Sultani aka'mpeleka watu wake ku angalia nani huyu. Akawaambia, mimi mtu kama watu. Wakamwambia, watoka wapi? Akawaambia, natoka mjini kwetu, nimekuja ku tembea, wakaenda wakamwambia mfalme, amekuja ku tembea mgeni. Akawaambia, enende mtu kesho amwambie Sultani atakuja kukutezama. Akaenda mtu, akamwambia. Akamwambia, marahaba, na aje.

Akaamrisha ku fanya vyakula vingi. Hatta assubui mfalme akaenda, na watu wake, akafika nyumbani. Aka'mkaribisha, akapita ndani, akaona Sultani nyumba kubwa na watumwa wengi ndani. Akakaa kitako, wakasumgumza. Akamwuliza, kwa nini huji mjini ku tembea? Akamwambia, mimi mgeni, sharti nipate watu wanitwae, wanipeleke mjini. Akamwambia, twende zetu, tukatembee.

Mfalme aka'mpenda sana, wakakaa siku nyingi pale. Mfalme akamwuliza, utake 'mke ku oa? Akamwambia, nataka. Akamwambia, nitakuoza mwanangu. Akafanya harusi kubwa Sultani akamwoza.

Akakaa na mkewe, akazaa mtoto 'mmoja, wa-

kakaa hatta hatima, yee na mkewe na mtoto wake 'mmoja na farasi yake, aka'mpenda kama roho yake.

## VITENDAWILI.

*Kitendawili!* ——— *Tega!*

Nyumba yangu kubwa, haina mlango!
YAYI.

Kuku wangu akazalia mibani!
NANASI.

Tandika kitanga, tule kunazi!
NYOTA.

Anatoka ku tembea anakuja nyumbani anamwambia, mama nieleke!
KITANDA.

Kombe ya Sultani i wazi!
KISIMA.

Watoto wangu wana vilemba, asio kilemba si mwanangu!
FUU.

## AO RATHI, AO MALI.

PALIKUWANA mtu mume na mkewe, wakaomba kwa Muungu ku pata kijana, wakapata wa kwanza manamume, na wa pili manamuke. Na baba yao, kazi yake ku chanja kuni. Wakakaa hatta wanakuwa waana wazima. Baba yao akashikwa na ugonjwa. Akawaita waanawe, akawauliza, wataka rathi, ao wataka mali? Yule manamume akamwambia, nataka mali. Manamuke akamwambia, nataka rathi. Aka'mpa rathi babaye sana. Babaye akafa.

Wakakaa matanga, hatta walipoondoka, mama yao akaugua, naye akawaita wanawe, akawaambia, wataka rathi, ao wataka mali? Mwanamume akamwambia, nataka mali. Na mwanamuke akamwambia, nataka rathi. Aka'mpa rathi mamaye yule. Akafa mama yao.

Wakakaa matanga, hatta alipoondoka ikipata siku ya saba. Akaenda mwanamume, akamwambia nduguye mwanamuke, toa vitu vyote vya baba yangu na mama yangu. Akatoa manamuke, asi'msazie kitu. Akachukua vyote.

Watu wakamwambia, huyu nduguyo mwanamuke humwachie walao kitu kidogo? Akanena,

sitamwachia, mimi nalitaka mali, yee akataka rathi. Akamwachia chungu na kinu, hatta chakula kidogo hakumwachia.

Wale jirani zake huja wakaazima kinu, wakatwangia, wakiisha, waka'mpa mchele kidogo, akapika, akala. Na wangine huja, wakaazima vyungu, wakapikia, wakiisha, waka'mpa naye chakula kidogo. Killa siku kazi yake ni hii.

Akatafutatafuta nyumbani mwa babaye na mamaye, asipate kitu, ela mbegu ya maboga. Akatwaa, akaenda, akapanda chini ya kisima. Ukaota mboga, ukazaa maboga mengi.

Yule nduguye hana habari, akauliza watu — chakula anapata wapi ndugu yangu? Wakamwambia, ku azima watu kinu, wakatwangia, waka'mpa naye chakula kidogo, na vyungu vyake ku azima watu, wakapikia, waka'mpa naye chakula.

Ndugu yake akaondoka, akaenda, aka'mnyang'anya kinu na vyungu. Amekwisha, aka'mka subui akatafuta chakula, hapati. Akakaa hatta saa tatu, akanena, nitakwenda ku angalia mboga wangu. umeota, Akaenda, akaona maboga mengi yamezaa. Akashukuru Muungu.

Akachuma maboga, akaenda, akauza, akapata chakula. Ikawa ndio kazi yake killa siku ku chuma, kaenda ku uza. Ikipata siku ya tatu,

killa mtu. aliokula maboga yale akaona matamu-'mno. Killa mtu huchukua nafaka wakamwendea pale pahali pake, wakanunua. Siku nyingi zimepita, akafanya mali.

'Mke wa ndugu yake akasikia habari ile, akatuma mtumwa wake na nafaka ku enda ku 'mnunulia boga. Akamwambia, yamekwisha, Alipojua mtumwa yule wa 'mke wa nduguye, akamwambia, twaa ile moja, 'mpelekee, na nafaka yako rudi nayo. Akaenda akalipika, akaona tamu'mno. Siku ya pili aka'mpeleka tena mtu. Akamwambia, hapana kabisa leo. Akaenda, aka-'mjibu bibi yake, akakasirika'mno.

Hatta mumewe alipokuja, akamwuuza, una nini mke wangu? Akamwambia, nimepeleka mtu kwa ndugu yako na nafaka yangu, ku enda ku taka maboga, hakuniletea, ameniambia, hakuna, na watu wote hununua kwake! Akamwambia mkewe, na tulale hatta kesho nitakwenda ku ng'oa mboga wake.

Hatta subui ku kicha akaenenda kwa nduguye, akamwambia, mke wangu ku leta nafaka ukakataa ku 'mliza boga. Akamwambia, yamekwisha, jana alileta mtu, nika'mpa burre. Akamwambia, mbona watu unawaliza? Akamwambia, yamekwisha, hakuna tena, hayajazaa. Ndugu

yake manamume akamwambia, nitakwenda ukata mboga wako. Akamwambia, huthubutu, labuda ukate mkono wangu kwanza, ndipo mboga uukate. Ndugu yake akakamata mkono wake wa ku ume, aka'mkata, akaenda akaukata na mboga wote pia.

Yule manamke akateleka maji ya moto, akatia mkono wake, akatia na dawa, akafunga kitambaa.

Aka'mnyang'anya vitu vyote, aka'mtoa na nyumba.

Akapotea yule nduguye ndani ya mwitu.

Nduguye huyu akauza nyumba, akakusanya mali mengi, akakaa akitumia.

Yule akapotea na mwitu, hatta siku ya saba akatokea 'mji mgine. Akapanda ju ya 'mti mkubwa, akila matunda ya mti, usiku hulala 'mle mtini. Hatta siku ya pili, akatokea kijana cha mfalme anapiga ndege, yee na watu wake. Hatta saa ya sita amechoka, akasema nitakwenda pale mtini, nikapumzike, na ninyi pigeni ndege. Akakaa chini ya mti, yee na mtumwa wake.

Yule kijana manamke akalia hatta machozi yakamwangukia mtoto wa mfalme chini. Akamwambia mtumwa wake, angalia nje, hakuna mvua? Akamwambia, hakuna, bwana. Akamw-

ambia, bassi, panda mtini uangalie ndege gani alionitia mavi. Akapanda mtumwa wake, akamwona mana'mke mzuri'mno analia, asimwambie neno, akashuka. Akamwambia bwana wake. huna kijana manamke mzuri'mno, sikuthubutu ku mwambia neno. Bwana wake akamwuliza, kwa nini? Akamwambia, nime'mkuta, analia, labuda wenda wewe. Akapanda bwana wake, akaenda, akamwona, akamwambia, una nini, bibi yangu, weye 'mtu, ao pepo? Akamwambia, mimi 'mtu. Akamwambia, unalilia nini? Akamwambia, nakumbuka ulimwengu, mimi ni 'mtu kana wewe.

Akamwambia, shuka, twende zetu kwetu. Akamwambia, kwenu wapi? Akamwambia, kwa baba yangu na mama yangu, mimi ni kijana cha mfalme. Akamwambia. umekuja fanya nini huku? Akamwambia, nimekuja ku piga ndege, mwezi hatta mwezi ndio kazi yetu, nimekuja na wenzangu wengi. Akamwambia, mimi sitaki ku onekana na mtu. Yule manamke amemwambia kijana cha mfalme. Akamwambia, hatuonekani na mtu. Akashuka chini.

Aka'mtuma mtumwa wake — enenda mjini upesi, ukaniletee machela. Akaenda mtumwa wake marra hiyo akarejea na machela na watu wanne, waka'mchukua. Aka'mtia manamke, aka-

mwambia, mtumwa wake, piga bunduki, wapate kuja jamaa yote. Akapiga bunduki, wakaja watu wenzi wake, wakamwambia, una nini, kijana cha mfalme? Akamwambia, na baridi, nataka kwenda zangu mjini. Wakachukua nyama iliopata, wakaenda zao. Na kijana cha mfalme ameingia ndani ya machera, yeye na yule kijana manamke. Na wale wenziwe hawana habari.

Wakaenda hatta mjini kwao, wakafikia nyumbani kwake. Akamwambia mtu — enenda kamwambia mama na baba, na homa leo, nataka uji upesi, waniletee. Wakafathaika mamaye na babaye, ukapikiwa uji, ukapelekewa.

Na babaye akaenda na mawiziri yake wakaenda ku'mtezama. Hatta usiku mamaye akaenda na watu wake ku'mtezama.

Hatta siku ya pili akatokea 'nje, akaenda, akamwambia mamaye na babaye, nimeokota kijana manamke nataka 'mnioze, walakini hana mkono moja. Wakamwambia, wa nini? Akawaambia, nataka vivyo hivyo. Na yule Sultani a'mpenda sana mwanawe 'mmoja tu, akafanya harusi, wakamwoza.

Watu wakapata habari mjini, mtoto wa Sultani ameoa kijana manamke, hana mkono moja.

Wakakaa kitako hatta mkewe akachukua mi-

mba, akazaa mtoto manamume, wakafurahi'mno wazee wake.

Yule kijana cha Sultani akasafiri, akaenda ku tembea katika miji ya baba yake.

Huku nyuma akatokea yule ndugu yake manamume, hana kitu cha ku tumia, anakwenda akiomba. Hatta siku moja, akasikia watu wanasumgumza — kijana cha mfalme ameoa manamke, hana mkono moja. Yule nduguye manamume akauliza, ame'mpata wapi kijana huyu mtoto wa mfalme? Wakamwambia, amemwokota mwituni. Aka'mjua kuwa nduguye.

Akaenda hatta kwa mfalme. Akaenda, akamwambia, mtoto wako ameoa mana'mke hana mkono moja, ametolewa huyu katika mji wao kwa sababu mchawi, killa mume anayemwoa humwua.

Na mfalme akaenda akamwambia mkewe, wakanena, ku fanya shauri gani? Nao wana'mpenda sana mtoto wao 'mmoja tu, wakasema, ku 'mtoa 'mji yule. Nduguye mwanamume akawaambia, mwueni, kwani uko kwao amekatwa mkono, na hapa mwueni. Wakamwambia, hatuwezi ku mwua, tuta'mtoa mji. Wakaenda, waka'mtoa mji, yeye na mwanawe. Akashukuru Muungu.

Akatoka, amechukua kitunga, akaenda zake, hatta mwituni, hajui anapokwenda, wala anako-

toka Akakaa kitako, akamwonyesha manawe, akitupa macho, akaona nyoka anakuja mbio hatta karibu yake, akanena, leo nimekufa.

Nyoka akamwambia, mwana Adamu, funua kitunga chako niingie, uniponye wa jua nitakuponya wa mvua. Akafunua, akaingia, akafunika. Akitezama, akaona nyoka mgine anakuja mbio, akamwambia, akupita mwenzangu? Akamwambia, huyu anakwenda. Akapita mbio.

Yule nyoka, aliomo kitungani, akamwambia, nifunua. Aka'mfunua, akashukuru Muungu, akamwambia yule mwana Adamu, unakwenda wapi weye? Akamwambia, sijui ninapokwenda, ninapotea katika mwitu. Akamwambia nyoka, fwata mimi, twende kwetu. Wakafwatana hatta njiani wakaona ziwa kubwa. Nyoka akamwambia, mwana Adamu, tukae tupumzike, jua kali, enenda kaoge ziwani na mtoto. Aka'mchukua kijana chake, akaenda ku mwosha, akatumbukia, aka'mpotea ziwani. Akamwuliza, una nini, mwana Adamu yuko? Akamwambia, mtoto wangu amepotea ndani ya maji. Akamwambia, 'mtafute sana. Aka'mtafuta saa mzima, asimwone. Akamwambia, tia mkono wa pili. Akamwambia, weye nyoka unanifanyia mzaha. Akamwuliza, kwa nini? Akamwambia, nimetia huu mzima, si-

kumwona, huu mbovu utafaa nini? Nyoka akamwambia, tia tu weye yote miwili. Akatia mwana Adamu, akaenda akamwona mwanawe, aka'mshika, aki'mtoa mkono wake mzima. Akamwambia, umemwona? Akamwambia, nimemwona na mkono wangu nimepata mzima. Akafnrahi sana.

Akamwambia nyoka, sasa twende zetu kwa wazee wangu, nikakulipe fathali yuko. Akamwambia, hii yatosha, ku pata mkono wangu. Akamwambia, bado, twende wazee wangu. Wakaenda hatta walipofika, wakafurahi sana, waka'mpenda yule kijana manamke. Akakaa kitako, akila, na ku lala, siku nyingi.

Yule mumewe akarudi ku tembea. Wale wazee wake wakafanyiza makaburi mawili, moja la mkewe, na moja la mtoto wake. Na yule ndugu yake manamume amekua mtu mkubwa kwa mfalme.

Akaja mumewe kijana cha mfalme. Akauliza mke wangu yuwapi? Wakamwambia, amekufa. Na mtoto wangu yuwapi? Waka'mjibu, amekufa. Akauliza, makaburi yao yakowapi? Waka'mpeleka ku enda ku yaona. Alipoona akalia sana. Akafanya matanga. Akashukuru Muungu.

Siku nyingi zimepita. Yule kijana mwanamke mwituni akamwambia rafiki yake nyoka, nataka kwenda zangu kwetu. Akamwambia, kamwage mama yangu na baba yangu, atakapokupa rukusa kwenda zako, wakikupa zawadi, usikubali ela pete ya baba na kijamanda cha mama.

Akaenda akawaga, waka'mpa mali mengi, akakataa akawaambia, mimi mtu 'mmoja nitachukuaje mali haya? Wakamwambia, wataka nini? Akamwambia, weye, baba, nataka pete yako, na weye, mama, nataka kijamanda chako. Wakasikitika'mno, wakamwuliza, aliokwambia nani habari hii? Akawaambia, mimi mwenyewe najua. Wakamwambia, hakuna, ni huyo nduguyo, aliokwambia.

Akatwaa pete, aka'mpa, akamwambia, pete hii nakupa, ukitaka chakula, ukitaka nguo, ukitaka nyumba ya ku lala, yambie pete, itakutolea, kwa rathi ya Muungu na mimi babayo. Na mamaye aka'mpa kijamanda, akamwambia vile vile. Waka'mpa na rathi.

Akatoka, akaenda zake, hatta kule mjini kwa mumewe, asifike nyumbani kwa mumewe. Akifika kiungani, akayambia pete, nataka utoe nyumba kubwa. Ikatoa nyumba, na pambo la nyumba, na watumwa. Akakaa kitako, yee na mwa-

nawe. Na mwanawe amekua kijana mkubwa.

Mfalme akapata habari, kuwa nyumba kubwa kiungani, akatuma watu ku enda ku tezama, waka'mjibu, kweli. Akaondoka Sultani na mawaziri yake na kijana chake.

Wakaenda, wakikaribia, akatezama durabini yule mana'mke, akamwona mumewe, na baba ya mumewe, na watu wengi, na yule nduguye yumo. Akawaambia watu, fanyeni vyakula upesi. Wakafanyiza, wakaandika meza. Wakafika, wakakaribishwa, wakaingia ndani, wakamwuliza, habari? Akamwambia, njema. Akawaambia, kaleni chakula, natoka mbali mimi, 'mkiisha chakula, niwape habari yangu.

Wakala chakula, hatta walipokwisha, akawaambia, toka mwanzo alipozawa, yeye na nduguye manamume, hatta yakaisha yote, kama yalipokuwa. Yule kijana cha mfalme akadnda ku'mkamata mkewe, wakalizana sana, na waliopo wote wakalia, wakajua kuwa nduguye manamume si mwema.

Mfalme akamwuliza, tu'mfanyieje nduguye mwanamume? Akamwambia, 'mtoeni 'mji tu. Akakaa na mumewe hatta hatima kwa furaha.

## KISA

## CHA HASSIBU KARIMI AD DINI NA SULTANI WA NYOKA.

ALIONDOKEA mtu mganga sana, akakaa, hatta mwana mtoto asipate, siku nyingi. Naye tabibu mkuu, haina dawa moja ya ulimwenguni asiyoijua. Na elimu nyingi anayoijua. Akakaa, hatta alipokuwa mzee sana mkewe akachukua mimba, naye hana kitu zayidi ya vyuo vya dawa.

Akaugua yule mtu, akamwita mkewe, akamwambia, nipe chuo changu, aka'mpa, akafunua akatezama ndani ya chuo, akamwambia, wewe una mimba, utazaa mtoto mwanamume, jina lake mwite Hassibu karimi ad dini. Akafa babaye.

Akakaa manamke, hatta akazaa mtoto mwanamume, aka'mlea, hatta akawa mkubwa

Yule mtoto akamwambia mamaye, jina langu nini? Akamwambia, ngoja, kesho tutafanya karamu, tutawaita watu, waje wale, nipate kukupa jina alionipa babayo.

Akakaa, assubui akafanya karamu kubwa, akawaita wanajimu, wakaja kula karamu, akawaambia, mtoto wenu leo nita'mpa jina alionipa babaye. Wakamwambia, 'mpe. Akawaambia, jina

lake, Hassibu karimi ad dini. Wakamwambia, heri.

Akatiwa chuoni ku soma, alipokwisha soma, akatiwa kiwandani ku shona nguo, asijue, akatiwa ku fua fetha, asijue, killa kazi anayofundishiwa hajui. Mamaye akanena, bassi, kaa kitako, mwanangu, akakaa kitako akila na ku lala.

Akamwambia, baba alikuwa na kazi gani? Akamwambia, alikuwa tabibu mkuu sana. Akamwambia, viwapi vyuo vyake vya utabibu? Akamwambia, siku nyingi zimepita, katezame ndani, kana viko. Akaenda, akatezama, akaona vimeliwa na wadudu, imesalia gombo moja, akatwaa, akasoma, akaona dawa zile zote.

Hatta siku hiyo wakaja jirani zake wakamwambia mamaye, utupe sisi huyu mtoto tukaende naye ku chanja kuni. Nao, wale watu wanne, kazi yao ku chanja kuni, wakija, wakiuza mjini. Nao hupakia kuni ju ya punda. Mamaye akawaambia, vema, kesho nita'mnunulia punda, 'mfuatane nyote.

Assubui mamaye aka'mnunulia punda, wakaja wale watu, wakafuatana naye kazini. Wakaenda, wakapata kuni nyingi, wakaja nazo mjini kuza, wakagawanya fetha.

Na siku ya pili wakaenda tena, na siku ya ta-

tu, na siku ya 'nne, na siku ya tanu, na siku ya sita. Hatta siku ya sabaa, walipokwenda, ku katanda wingu, ikanya mvua, wakakimbia ku jificha chini ya jabali.

Yule Hassibu amekaa mahala pekeyake. Akatwaa jiwe, akagonga chini, akasikia panalia wazi, akawaita wenziwe, akawaambia, hapa panalia wazi!

Wakamwambia, gonga, akagonga, wakasikia panalia wazi, wakamwambia, tuchimbe. Wakachimba, wakaona shimo kubwa, limekaa kana kisima, wakaangalia ndani 'mna asali, limejaa tele.

Wakaacha kuni, ikawa ku chukua asali, kulla siku. Na yule Hassibu ndiye, aliyeliona mbele ile shimo la asali. Wakamwambia, wewe ingia 'mmo ndani, ukiteka asali, ukatupa sisi, tukaende tukauze mjini, hatta tukiisha, tupate ku gawanya fetha. Akanena, vema.

Ikawa kazi zao kulla siku miezi mitatu, wakapata mali mengi.

Hatta asali ilipokwisha, imesalia chini kabisa nako mbali, wakamwambia, ingia wewe, ndani kule, ukwanguwe iliosalia chini, ukiisha, tutakupa kamba, ushike, tukupandishe ju. Yule akakubali, akakusanya, akawaambia, nipeni kamba. wakawaambia, hapana kamba, ngoja kwanza, i-

nakuja. Wakafanya shauri, wakasema, huyu na tu'mwache mumo humo ndani ya shimo, tugawanye sisi mali.

Akaondoka 'mmoja, akasema, mama yake. tutamwambiaje? Akaondoka 'mmoja, akajibu, akamwambia, tutamwambia, mtoto wako aliondoka, kwenda chooni, akakamatwa na simba, yeye na punda wake, nako ndani ya mwitu tusiweze ku'mtafuta sana, lakini tukasikia simba analia, tukajua aliye'mkamata ni yeye simba.

Wakaenda zao mjini. wakamwambia mamaye, Mamaye akalia sana, akakaa matanga, hatta yakaisha. Wale wakagawanya fetha, wakasema, tu'mpelekee na mama ya rafiki yetu kidogo fetha, waka'mpelekea.

Bassi kulla siku, yule hu'mpelekea mchele, yule hu'mpelekea mafuta, hu'mpelekea kitoweo, hu'mpelekea nguo, kulla siku.

Bassi hapa, turejee aliko Hassibu.

Amekaa siku ya kwanza, siku ya pili, siku ya tatu, akajua wenziwe wame'mtupa, akashukuru Muungu. Akatembea ndani ya shimo, shimo kubwa sana. Usiku hulala 'mle'mle, assubui akia'mka, hupata asali kidogo, akala. Hatta siku moja amekaa kitako anawaza, akaona 'nge akaanguka chini, mkubwa sana, akamwua.

Akakaa kitako, akafikiri, 'nge huyu anatoka wapi? Labuda pana tundu mahala, nitakwenda kutafuta. Akaenda, akaona tundu ndogo, aona mwangaza mbali sana, akachokora kwa kisu, ikawa tundu pana sana, akapita, anaona mbali weupe na mwangaza, akaenda. Hatta akifika, akaona kiwanja, ametokea mahala pakubwa sana.

Akaona njia, akafuata njia, akaenda, akaona nyumba kubwa ya mawe, akaona na viti vingi, na mlango wake wa thahabu, na kufuli yake ya thahabu, na ufunguo wake wa lulu, akatwaa, akafungua, ndani akaona sébule kubwa, na viti vingi, akaona kiti kimoja cha thahabu, kimenakishiwa kwa lulu na jawahir na fusfús, akaona na kitanda kimetandikwa sana vizuri, akaenda akalala.

Hatta marra hiyo asikia watu wanakuja wengi. Wakaja hatta nyumbani, wakaona mlango umefunguliwa, wakaingia ndani. Na yule anayekuja ndiye Sultani wa nyoka.

Asikari wake wakajaa uwanjani, yee na mawaziri wake wakapita ndani, wakaona ajabu, wakamwona mtu amelala ju ya kitanda, na kile ndicho kitanda cha Sultani, anachokaa. Wakataka kumwua, akawaambia, 'mwacheni, 'msimwue, niwekeni kitini, waka'mweka ju ya kiti.

Akawaambia, mwamusheni polepole, waka-

mwamusha. Akaondoka, akakaa kitako, akaona nyoka wengi, wame'mzunguka, akamwona yule 'mmoja mzuri sana, amevaa nguo za kifaume.

Akamwuliza, wewe nani? Akamwambia, mimi Sultani wa nyoka, na hii nyumba yangu; akamwuliza, na wewe nani? Akamwambia, mimi Hassibu karim ad dini. Watoka wapi? Akamwambia, sijui ninapotoka wala ninakokwenda. Akamwambia, starehe; akawaambia asikari wake, enendeni mukalete matunda yote mwituni, tu'mkerimu mgeni.

Wakaenda, wakaleta kulla tunda, waka'mwekea mbele sinia nzima, wakamwambia kula. Akala hatta akashiba, waka'mpa maji, akanywa. Bassi, akakaa kitako, wakasumgumza.

Yule Sultani wa nyoka akamwuliza Hassibu, nipe kisa chako, toka ulipotoka kwenu hatta leo. Aka'mpa kissa chote kilicho'mpata njiani hatta akafika pale.

Naye Hassibu karim ad dini akamwuliza Sultani wa nyoka unipe kisa chako nawe, nipate ku jua. Akamwambia kisa changu kikubwa sana.

Akamwambia, nalikaa zamani moja, tukaondoka hapa kwenda jabali Al Káff, kwenda ku badili hawa. Nikakaa hatta siku moja nikamwona mtu akija. nikamwuliza, watoka wapi wee?

Akaniambia, mimi natoka mjini kwetu, ninapotea katika barra. Nikamwambia, weye mtoto wa nani? Akaniambia, mimi jina langu Bolukia, na baba yangu Sultani amekufa, nikaenda ku fungua kasha, nikaona mkoba, nikaufungua, umetiwa kisanduku cha shaba, nikafungua, ndani umefungwa kwa joho, nikafunua joho, nikaona chuo, nikasoma mimi, nikaona sifa nyingi za mtume. Nikafanya shauko kumwona mtu huyu. Nikawauliza watu, wakaniambia bado hajazaliwa. Nikasema, mimi nitapotea hatta nimwone. Nikaacha mji wangu na mali yangu, ni katika ku potea hatta sasa sijamwona mtu huyo.

Na mimi nikamwambia, utamwona wapi hajazaliwa bado? Labuda ungalipata maji ya nyoka, ungaliweza ku ishi, usife, hatta ukaonana naye, lakini sasa haifai, yako mbali maji ya nyoka.

Akaniambia, kua heri tena, nitapotea mimi. Nikamwambia, kua heri. Akaenda zake.

Hatta akafika Misri, akamwona mtu, akamwuliza, weye nani? Akamwambia, mimi Bolukia. Akamwuliza, na weye nani? Akamwambia, mimi jinalangu Alfán. Akamwambia, unakwenda wapi? Akamwambia, mimi nimeacha mji wangu na ufalme wangu na mali yangu, na'mtafuta mtume.

Akamwambia, utamwona wapi weye. naye hajazaliwa bado? Lakini sasa tuka'mtafute Sultani wa nyoka, tuki'mpata huyu, atatupa dawa sisi tutakwenda hatta alipo nebii Sulimani; tutapata pete yake, tutawale sisi na majini yote, yetakuwa chini yetu, tutakalo tutawaa'mru.

Akamwambia, mimi nimemwona Sultani wa nyoka katika jabali Al Káf. Akamwambia, twenende bass. Na yule Alfán moyoni mwake anataka pete ya nabii Sulimani apate ku tawala, yee awe mfalme wa Majini na ndege. Yule Bolukia ataka kumwona mtume, ndio shauko yake.

Alfán akamwambia Bolukia, sasa tufanye tundu ya ku 'mtegea Sultani wa nyoka, akiisha ingia ndani ya tundu, tulifunge, tu'mchukue.

Akamwambia, haya. Akafanya tundu, akitia vikombe viwili, kimoja cha maziwa, kimoja cha mvinyo. Wakaenda hatta wakafika jabalini.

Nipo sijaondoka bado kwenda mjini kwangu. Wakaenda, wakaweka tundu ile. nikaingia ndani nikanywa mvinyo, nikanilevya, wakanifunga, wakanichukua.

Hatta nilipoa'mka, naona nimechukuliwa na watu, na yule Bolukia yuko ndiye alionichukua. Nikanena, waana Adamu si wema, wataka nini sasa? Wakaniambia, twataka dawa tupake mi-

guuni mwetu, tukanyage bahari hatta tufike tunakotaka. Nikawaambia, twendeni.

Wakaenda nami hatta kisiwani, na kisiwa kile kina miti mingi. Na ile miti ikiniona hunena yote — mimi dawa ya fullani — mimi dawa ya fullani — mimi dawa ya kitwa — mimi dawa ya miguu — hatta ule mti ukasema, mimi, mtu akipaka miguuni hupita ju ya bahari.

Wakanena, ndio tutakao. Wakatwaa mwingi. Wakarudi, wakanipeleka hatta pale jabalini. Wakanifuungu., wakaniachia. Wakaniambia, kua heri, nikawaambia, kuaherini.

Wakaenda zao, wakipata bahari hupaka miguuni, wakapita. Wakaenda vivyo hivyo hatta wakafika siku nyingi sana wakakaribia alipolala nabii Sulimani mahala karibu Alfán akafanya madawa yake, wakaenenda.

Naye nabii Sulimani anangojewa na majini. wakakaribia wale wawili, wakasikia mtu anasema. Na nabii Sulimani amelala na mkono ameuweka kifuani, na pete kidoleni. Yule mtu akamwambia, akamwita Bolukia, unakwenda wapi weye? Akamwambia, nimefuatana na Alfán, anakwenda twaa pete ile. Akamwambia, rudi weye, huyu atakufa.

Alfán akamwambia Bolukia, ningoje hapa we-

ye. Akaenda yee, akikaribia ku taka ku shika pete, akapigiwa ukelele, akarushwa hapa hatta kule. Akarudi, asikubali, akaenda marra ya pili akataka kuishika pete, akapuziwa, akateketea kamma jifu.

Na yule Bolukia anaona pia, akasikia mtu akimwambia, rudi, enda zako, huyu thalimu amekwisha kufa.

Akarudi Bolukia, akaja zake hatta njiani akaona bahari, akapaka dawa yake miguuni, akavuka, akaenda kisiwa kingine, hatta akaisha akapaka dawa tena akavuka. Ikawa ndio kazi yake siku nyingi sana, na miezi mingi, na miaka mingi inakwisha naye njiani.

Akaenda hatta siku moja aka'mtokea mtu, akamwona amekaa kitako, aka'mpa salaam, naye aka'mjibu. Akamwuliza, weye nani? Akamwambia, mimi, jina langu. Jani Shah, weye nani? Akamwambia, mimi Bolukia, akamwuliza, wafanya nini hapa?

Pana makaburi mawili, na yule mtu amekaa katikati ya makaburi. hulia sana, kiisha akacheka, akashukuru Muungu. Akamwuliza, nipe kisa chako wewe. Akamwambia, kisa changu kikubwa, lakini nipe chako weye kwanza, umetoka wapi, unakwenda wapi?

Akamwambia, miye ni mtoto wa Sultani, baba yangu amekufa, nimetawala mimi. Hatta siku moja nikafungua kasha la baba, nikaona mkoba, ndani na chuo, nikasoma chuo kile, nikaona sifa za mtume, nikafanya shauko sana ya ku mwona, nikatoka mimi katika mji wangu, nikapotea katika mwitu ku 'mtafuta mtu huyo. Na kulla mtu nimwonaye huniambia, hajazaliwa bado. Na hatta sasa ni katika 'mtafuta bado. Nikali nikienda katika barra.

Akamwambia, kaa kitako bassi, nikupe kisa changu toka mwanzo hatta sasa. Akamwambia, nipe, nimekwisha kaa kitako.

Akamwambia, mimi, jina langu Jani Shah, na baba yangu, jina lake Taighamusi, Sultani mkubwa. Naye kulla siku ikipata mwezi huenda mwituni kwenda ku piga nyama. Na mwanawe ni mimi tu 'mmoja, anipenda sana. Hatta siku hiyo nikamwambia, baba, tufuatane mwituni. Akaniambia, kaa kitako, usiende mahali. Nikalia sana mimi, baba yangu akaniambia, twende, usilie.

Tukaenda zetu mwituni, na watu wengi wanaokwenda. Hatta tulipofika mwituni tukala chakula, tukaisha, bassi kulla mtu tukaingia mwituni tupige nyama.

Na mimi na watumwa wangu, watu sabaa, tu-

kaenda njia yetu ngine, hatta tukifika mwituni, tukaona paa mzuri'mno, tuka'mfukuza hatta baharini, tusi'mpate. Akaingia majini paa, tukatwaa mashua, tukaingia mimi na watumwa wangu watu wanne, wale watatu wakarudi kwa baba. Sisi tuka'mfukuza paa hatta tusiuone mji, tuka'mkamata paa, tuka'mchinja. Tulipokwisha 'mchinja, ukavuma upepo mwingi, tukapotea.

Wale watumwa, wale watatu, walipofika kwa baba yangu, akawauliza, yuwapi bwana wenu? Wakamwambia, twali'mfukuza paa, hatta tukafika pwani, yule paa akaingia baharini, wakaingia mashuani, yee bwana na watu wanne, waka'mfukuza, sisi tukarudi.

Baba yangu akasema, mwanangu amekwisha potea. Akaenda zake mjini, akakaa matanga, akashukuru Muungu.

Sisi tukaangukia kisiwani. Pana ndege wengi. Tukatafuta matunda tukala, tukatafuta na maji tukanywa. Hatta usiku, tukapanda ju ya mti tukalala. Alfajiri tukaingia mashuani mwetu, tukapotea, tukafika kisiwa kingine cha pili, hapana mtu awaye yote. Tukashuka, tukala matunda mengi, hatta usiku tukapanda ju ya mti, tukalala, wakaja nyama mbwayi, wakacheza sana.

Hatta assubui tukakimbia, tukaenda kisiwa

cha tatu, tukifika tukitafuta matunda, tukaona mtofaa umezaa sana. Tukitaka ku chuma, tukasikia mtu, akatukataza, akinena 'msichume, mtofaa u wa mwenyewe mfalme, nimewekwa ku ungojea. Hatta usiku, wakaja kima wengi, wakafurahi sana walipotuona sisi, wakatutafutia matunda wakaletea, tukaja, tukala, hatta tukashiba.

Wakasema, mtu huyu tu'mfanye Sultani wetu. Yule 'mmoja akanena, watakimbia assubui hawa. Wakasema, kaivunjeni mashua yao. Wakaenda, wakaivunja.

Hatta assubui tukiondoka ku kimbia, tukaenenda pwani, mashua yetu imevunjwa. Bassi, tukarudi, tukakaa kitako, wakatuletea chakula, tukala, na maji, tukanwa. Na wale kima wanatupenda sana sisi, hawatupendi ku ondoka. Siku nyingi tukakaa.

Hatta siku moja tukaenda ku tembea, tukaona nyumba kubwa ya mawe, na mlango wakwe umeandikwa. Nikasoma mimi, ya kwamba, mtu anaokuja hapa kisiwani, hawa kima hawamwachi ku'mpenda'mno 'mfanya ndio mfalme wao. Na atakapokwenda zake, hapati njia, lakini iko njia moja, imelekea kibula, hufuata njia hiyo, hutaona uwanja mkubwa, una simba na chui na nyoka, 'mtapigana nao, 'mkiwashinda, 'mtapata njia, 'm-

takwenda mbele, 'mtaona uwanja mgine, una tungu wakubwa, kana umbwa, na meno yao kana umbwa, wakali sana, 'mtapigana nao, 'mkiwashinda, 'mtapata njia ya ku pita.

Tukafanya mashauri, wale watumwa wangu wakaniambia, tuenende, tukapone ao tukafe, na sisi sote tuna selaha zetu.

Tukaenenda hatta tukafika uwanja wa kwanza, tukapigana, wakafa watumwa wangu wawili. Tukaenda zetu, tukapita, tukaenda wa pili, tukapigana, wakafa watumwa wangu wawili, nikapona mimi.

Nikapotea siku nyingi, hatta nikatokea mji. Nikakaa kitako pale mjini, natafuta kazi, sipati. Akatokea mtu, akaniambia, wataka kazi? Nikamwambia, nataka. Akaniambia, twende zetu, tukaenda kwake.

Akachinja ngamia, akatwaa ngozi ile, akaniambia, nitakutia ndani ya ngozi, wende ju ya jabali, ndege atakuchukua, ukifika atakufungua, usukume vito chini, ukiisha nitakushusha mimi.

Akanitia ngozi ile, akaja ndege, akanichukua akaniweka ju ya jabali, akataka ku nila, nikaondoka, nika'mfukuza ndege, akaruka. Nikasukuma vito chini vingi, nikamwambia, nishushe, bass! Asinijibu neno, akaenda zake.

Nikasema, nimekufa mimi. Nikaenenda mwituni siku nyingi. Nikatokea nyumba moja, nikamwona mzee katika nyumba, akanipa chakula na maji, nikashukuru Muungu.

Nikakaa kitako pale, akanipenda kana mwanawe. Akanipa funguo zote za nyumba, akaniambia, fungua kulla utakapo, ela chumba hiki kimoja usifungue. Nikamwambia, vema, baba.

Nikakaa, akatoka yee kwenda ku tembea, nikafungua mimi, nikaona bustani kubwa, na mto unapita. Marra wakaja ndege watatu, wakatua pale mtoni. Marra wakageuka watu, wakaoga mtoni, na wazuri'mno wale watatu waanawake. Nikawatezama hatta walipokwisha ku oga, wakavaa nguo zao, wakaruka.

Nikarudi mimi, nikafunga mlango, nisiweze kula kitu. Hatta baba yangu akaja, akaniuliza una nini? Nikamwambia, nimekwenda katika bustani, nimeona waanawake watatu, wamekuja ku oga, wamekwisha, wameruka, na yule 'mmoja na'mpenda'mno, nataka kumwoa, kama siku'mpata nitakufa.

Akaniambia, wale hawapatikani, wale watoto wa Sultani wa majini, na kwao mbali sana, mwendo miaka mitatu. Nikamwambia, sijui, sharti unipatie, akaniambia, ngoja marra hii, watakapo-

kuja ku oga, ujifiche, utwae nguo za yule u'mpendaye sana.

Nikaenda nikangoja, hatta walipokuja wakavua nguo zao. nikazitwaa, nikazificha. Na yule ndio mdogo wao, na jina lake Seyedati Shemsi. Walipotoka wakavaa nguo zao, wale nduguze, yee akatafuta zake, asizione. Nikamwambia, ninazo mimi. Akaniambia, nipe mwenyewe, nataka ku enda zangu. Nikamwambia, mimi nakupenda sana, nataka kukuoa. Nataka kwenda kwa baba yangu. Nikamwambia, huendi.

Wakaruka wale nduguze, wakaenda zao, nika'mchukua kwetu, yule baba yangu akanioza. Akaniambia, nguo hizi usi'mpe, zifiche sana, akizipata mwenyewe, ataruka kwenda zake kwao. Nikazichimbia chini, nikazitia.

Hatta siku hiyo nimetoka kwenda ku tembea, akazifukua, akazivaa mwenyewe akaruka, akakaa ju ya dari, akamwambia mtumwa wake, bwana wako akija mwambia nimekwenda zangu kwetu, kama anipenda anifuate. Akaruka, akaenda zake.

Hatta nilipokuja, nikaambiwa, mkewo amekwenda zake kwao. Nikapotea niki'fuata miaka mingi.

Hatta nilipofika karibu na mji nikaona watu,

wakaniuliza, weye nani? Nikawaambia, mimi Jani Shah. Mtoto wa nani? Nikawaambia, mtoto wa Taighamusi. Wakaniambia, weye ndiye uliye umeoa bibi yetu? Nikawauliza, nani bibi yenu? Wakaniambia, Seyedati Shemsi. Nikawaambia, miye. Moyo wangu ukafurahi sana.

Wakanichukua hatta mjini kwao. Akamwambia babaye, huyu ndio mume wangu aliyenioa. nikapendwa sana, nikakaa siku nyingi.

Babaye akaniambia, 'mchukua mkewo, kama wataka kwenda kwenu. Tukapewa Majini, wakatuchukua kwa siku tatu. Tukafika, tukakaa mwaka.

Nikasema, twende, tuangalie baba yetu. Mke wangu akaniambia, twende. Hatta tukifika hapa, mke wangu akaenda ku oga. Hatta akitoka, amekufa, nika'mzika hapa. Wale Majini wakaenda kwa babaye kumwambia, mwanawo amekufa. Babaye akasema, kamwiteni Jani Shah, aje, aoe huyu mtoto mgine. Wakaja kuniambia. Nimesema, sitaki, nitachimba kaburi la pili, nikifa, niingie ndani. Ndio kisa changu.

Akakaa hatta akafa. Na yule Bolukia akaenda zake, akafa njiani.

Sultani wa nyoka akamwambia Hassibu, na wewe ukienda kwenu utanifanya vibaya. Aka-

mwambia, sitakufanya vibaya, nipeleke kwetu. Akamwambia, miye najua, nikikupeleka kwenu, utarudi, uje, uniue. Akamwambia, sithubutu, nipe kiapo, niape. Aka'mpa watu, waka'mpeleka kwao. Akamwambia, ukifika kwenu, usiende ku oga panapo watu wengi. Akamwambia, siendi. Waka'mpeleka kwao, hatta walipofika, wakarudi wale, wakamwambia, kua heri. Akaenda kwa mamaye, akafurahi sana mamaye.

Na 'mle mjini mwao, Sultani hawezi sana, na dawa yake sharuti apatikane Sultani wa nyoka, auawe, nyama yake itokoswe, ndio dawa.

Yule waziri akaweka watu katika hamami, akawaambia, akija mtu ku oga ana alama tumboni 'mkamateni.

Yule Hassibu akakaa siku tatu, akasahao maneno ya yule rafiki yake Sultani wa nyoka, akaenda ku oga.

Wale asikari waka'mkamata, waka'mpeleka kwa waziri. Waziri akamwambia, utupeleke mahala alipokaa Sultani wa nyoka. Akamwambia, sipajui. Akawaambia, 'mfungeni. Akafungwa akapigwa sana, akapasukapasuka maongoni. Akawaambia, nifungueni, niwapeleke.

Wakafuatana, wakaenda, hatta walipofika, Sultani wa nyoka akamwambia, sikukwambia, u-

takuja niua? Akamwambia, si mimi, na angalia maongoni mwangu. Akamwuliza, nani amekupiga hivi? Akamwambia, waziri. Akamwambia, bassi, sasa mimi nimekwisha kufa, lakini sharti unichukue wewe hatta kwenu. Aka'mchukua, na wale asikari wakarudi, na yule waziri yumo 'mle'mle.

Akamwambia njiani rafiki yake, mimi nikifika nitauawa, na nyama yangu itapikwa, povu la kwanza, waziri atakwambia kunywa wewe, nawe usinywe, litie chupani, u'mwekee, la pili kunywa wewe, utakuwa tabibu mkubwa, la tatu ndio dawa la Sultani wenu. Na hili la kwanza akija akikuuliza, umekunywa wewe la kwanza? Mwambie, nimekunywa, na hili la pili lako weye. Waziri atapokea, akiisha kunywa, atakufa, utapumzika roho yako.

Wakaenda zao, hatta wakafika mjini, wakafanyiza vilevile kama alipomwagiza rafiki yake.

Yule waziri akanywa, akafa, na lile la pili akanywa yeye, na la tatu aka'mfanyia dawa la Sultani, akapona.

Aka'mpenda sana Sultani, akawa tabibu mkubwa katika mji, akakaa raha kwa uzima hatta khatima.

## MTU AYARI NA HAMALI.

MTU alikuwa ayari, huenda sokoni akinunua vitu, akiisha nunua wale watwekao hawapi ujira wao.

Siku moja akanunua sanduku ya bilauri, akatafuta mtu wa ku 'mchukulia, akapata hamali akamwambia, katika mambo mawili khitari mojawapo, kukupa ujira wako, ao nitakupa maneno matatu ya ku kufaa ulimwenguni. Akamwambia, mapesa napata killa siku, nitakuchukulia kwa haya maneno matatu, utakayoniambia.

Akachukua sanduku. Akipata thulúth ya njia akamwambia, bwana wangu, sanduku hili zito, limenilemea, nipe neno moja, nipate ku pata afia za ku enenda.

Akamwambia, mtu akikwambia, utumwa bora kuliko ungwana, usi'msadiki.

Akamwangalia sana, aka'mjua, huyu mwenyi sanduku hii ni ayari, lakini ni kheri nisubiri hatta nifike. Wakaenenda, wakipata thulúth ya pili, akamwambia, niambie neno la pili.

Akamwambia, mtu akikwambia, umasikini ni bora kuliko utajiri, usi'msadiki.

Wakaenenda hatta walipofika nyumbani. Akamwambia, bwana niambie neno la tatu. Akamwambia, tua. Akamwambia, nina furaha'mno kwa yale maneno mawili ulioniambia, niambie la tatu, nipate ku tua.

Akamwambia, mtu akikwambia, njaa ni bora kuliko shiba, usi'msadiki.

Akamwambia, jitenge, bwana, nilitue. Akainua ju ya kitwa, akalipomosha. Mwenyewe akamwambia, a-a-a umenivunjia sanduku yangu?

Akamwambia, na mtu akikwambia, imesalia bilauri moja katika sanduku hii haikuvunjika, nawe usi'msadiki.

---

## UTUMBUIZO WA GUNGU.

### GUNGU LA KU FUNDA.

PANI kiti, nikae kitako,
Tumbuize wangu Mananazi,
Tumbuize wangu mana'mke,
'Mpanguwa hamu na simanzi.
Husimama tini wa mlango
Kiwa nde kwenda matembezi,

Chiwa nde kaingia shughuli,
Kiwaambia wakwe waandazi,
Kamwambia Sada na Rehema
Mwandani pasiwa ajizi,
Wandani, tendani haraka,
Mwandae wali na mtuzi.
Akimbona nimelimatia,
Kaondoa chakwe kiyakazi,
Mwangalie usita wa yumbe,
Ao kwao kwa fumo wa ezi,
Mwangalie tengoni pa nduze,
Ao kwao kwa mama shangazi,
Ka'mpate, hima uye naye.
Watendani hatta njeu shizi,
Kamwambia, bwana, waamkuwa,
Tenda hima, sifanye ajizi,
Yanga lako wimie tutule,
Na matoni hutuza tozi.
Kaamba tende tangulia, naja,
Ka'mtuze, ate simanzi,
Kamwandama nyuma kiongoya,
Akinuka meski na mbazi.
Akiingia ka'mpa salamu,
Ka'mjibu mwana wa Hejazi.
Saa hiyo kaondoka akaima,
Kamwandika mkono wa fuzi,

Kamwombea Muungu Jabari,
Ewe mama, Mola ngwakujazi.
Akiinua mkonowe mwana
Kaupeeka ju la mwanzi.
Akaangua kisuto cha kaye,
Cha kinisi chema matorazi,
Ka'mweka kituzo cha mato.
Buni ami, mwana wa shangazi,
Kimwambia, bwana na tukae,
Siime'mno, ukataajazi.
Nitiani hoyo Timi aye,
Na anguse, ate masindisi,
Apakue pilao ya Hindi,
Mzababu isiyo mtuzi.
Ete kiti chema cha Ulaya,
Na sinia njema ya Shirazi
Munakashi inakishiweyo,
Na sahani hung'ara ja mwezi.
Kaamuru khodama na waja,
Ai nini ha'mtumbuizi?
Bassi hapo akamwandikia
Naye Timi yushishiye kuzi,
Yapejeto maji ya zabibu
Ki'mnyesha kama 'mna shizi.
Ki'mlisha aki'mrehebu
Kimwonya kwema maozi.

Ki'mlisha tambuu ya Siu,
Ya layini layini ya Ozi,
Kiukuta kuno kimwakiza,
Kwa iliki pamwe na jozi.
Nikumele ku sifu mbeja
Mteule wangu Mananazi.

GUNGU LA KU KWAA.

MAMA, nipeeke, haoe kaoe
Urembo na shani Ungama,
Haoe mnara mpambe mpambe,
Uzainyeo heshima.
Na wenyi ku pamba patoto patoto.
Wavete vitindi na kama,
Wavete saufo ziemba ziemba,
Na mikili bee na nyuma.
Wavete libasi teule teule,
Kwa zitwana bee na nyuma.
Watukuze panga na ngao na ngao.
Mtu hutoshea ku ona.
Kujile Mngazidja na kubu na kubu,
Ujile ku taka harubu.
Kujile Mgala na mata na mata,
Ujile ku taka ku teta.
Tutawatilia ukuta ukuta,
Wasituingilie myini.

## HADITHI YA LIONGO.

HAPO zamani za Shanga palikuwa mtu, jina lake Liongo, naye ana nguvu sana, mtu mkubwa sana katika mji. Akauthi'mno watu, hatta siku hiyo, wakafanya shauri kumwendea nyumbani kwake ku'mfunga. Wakaenda watu wengi sana waka'mingilia nyumbani gháfula, waka'mkamata waka'mfunga, wakaenda naye hatta gerezani, waka'mtia.

Akakaa siku nyingi, akafanya hila hatta ku fungua. Akatoka nje, akauthi watu vilevile, siku nyingi. Watu hawawezi kwenda mashamba, wala ku kata kuni, wala ku teka maji. Wakauthika sana.

Watu wakasema, tufanye hila gani, hatta tu'mpate, tumwue? Akanena 'mmoja, tumwendee anapolala, tumwulie mbali. Wakasema wangine, 'mki'mpata, 'mfungeni, 'm'mlete. Wakaenda wakafanya hila, hatta waka'mpata, waka'mfunga, waka'mchukua mjini. Wakaenda waka'mfunga mnyororo, na pingu, na mti kati.

Wakamwacha siku nyingi, na mamaye hu'mpelekea kula kulla siku. Na mbele ya mlango

kule alikofungwa, wamewekwa asikari wanayo-'mngojea, hawaondoki marra moja ela kwa zamu.

Siku nyingi na miezi mingi imepita. Kulla siku, usiku usiku, kuimba nyimbo nzuri, kulla asikiaye huzipenda sana zile nyimbo. Kulla mtu humwambia rafiki yake, twende tukasikilize nyimbo za Liongo, anazokwimba chumbani. Huenenda, wakisikiliza. Kulla siku ikipata usiku, huenda watu, wakamwambia, tumekuja kwimba nyimbo zako, tusikie. Huimba, hawezi ku kataa, wakazipenda'mno watu mjini. Na kulla siku ku tunga nyingine nyingine kwa sikitiko la ku fungwa. Hatta watu wamezijua nyimbo zile kidogo kidogo, lakini yeye, na mamaye, na mtumwa wake wanazijua sana. Na maana yake zile nyimbo mamaye azijua, na wale watu mjini hawajui maana yake.

Hatta siku hiyo kijakazi chao ameleta chakula waka'mnyang'anya wale asikari, wakala, waka'msazia makombo, waka'mpa. Yule kijakazi akamwambia bwana wake, nimeleta chakula, wameninyang'anya hawa asikari, wamekula, wamesaza haya makombo. Akamwambia, nipe. Akapokea, akala, akashukuru Muungu kwa yale yalio-'mpata.

Akamwambia kijakazi chake, (na yeye ndani

na kijakazi yu nje ya mlango)

Ewe kijakazi nakutuma uwatumika,
Kamwambia mama, ni mwinga siyali'mka,
Afanye mkate, pale kati tupa kaweka,
Nikeze pingu na minyoo ikinyoka,
Ningie ondoni ninyinyiririke ja mana nyoka,
Tatange madari na makuta kuno kimeta.

Maana yake — Wee kijakazi utatumika kamwambia mama, ni mjinga sijaerevuka, afanye mkate, katikati aweke tupa nikate pingu, na minyololo ikifunguke, niingie njiani, niteleze kama nyoka, nipande madari na kuta, nikitezama huko na huko.

Akamwambia, salaam sana mama, mwambie kama haya niliokwambia. Akaenda, akamwabia mamaye, akamwambia, salaam sana mwanao, ameniambia maneno kuja kukwambia. Akamwambia, maneno gani? Akamwambia, kama yale yalioambiwa.

Mamaye akajua, akaenda zake dukani, akabadili mtama, aka'mpa mtumwa wake ku twanga. Yeye akaenda ku nunua tupa nyingi, akaleta. Akatwaa unga ule, akafanya mikate mizuri mingi. Akatwaa chachu, akafanya mkate mkubwa, akatwaa tupa akatia ndani, aka'mpa mtumwa wake, ku'mpelekea.

Akaenda nao, akifika m'langoni asikari waka-'mnyang'anya, wakachegua mikate mizuri, wakala wao. Ule wa chachu wakamwambia, 'mpelekea bwana wako. Yule aka'mpelekea, akauvunja, akatoa tupa zile akaziweka, akala mkate huu akanywa maji, akashukuru Muungu.

Na wale watu mjini wataka auawe. Mwenyewe akasikia ya kuwa ya kwamba atauawa. Akawaambia asikari, nitauawa lini? Wakamwambia, kesho. Akawaambia, kanitieni mama yangu na mwenyi mji, na watu mjini wote, nije niagane nao.

Wakaenda, wakawaita, wakaja watu wengi wote, na mama yake na yule mtumwa wake.

Akawauliza, 'mmekutanika nyote? Waka'mjibu, tumekutanika. Akawaambia, nataka pembe, na matoazi, na upato, zikaenda zikatwaliwa. Akawaambia, na machezo leo nataka ku agana nanyi, wakamwambia, vema, haya, piga. Akawaambia, 'mmoja ashike pembe, na 'mmoja ashike matoazi, na 'mmoja ashike upato. Wakamwambia, tupigeje? Akawafundisha ku piga, wakapiga.

Naye mwenyewe ndani kule aliko akaimba, hatta iliposita wi ngoma, akashika tupa, akakata pingu. Ile ngoma ikinyamaa naye hunyamaa, a-

kaimba, wakipiga, yeye akakata pingu.

Na watu wale hawana khabari ilioko ndani, hatta ikakatika pingu, akakata na mnyororo hatta ukakatika. Na wale watu hawana khabari kwa shauku ya ngoma. Wakitahamaka amevunja mlango amewatokea nje. Wakitupa vitu hivi kwenda mbio wasidiriki akawakamata akawapiga vitwa kwa vitwa akiwaua. Akitokea nje ya mji, akaagana na mamaye "kutuonana tena."

Akaenda zake mwituni akakaa kitako siku nyingi huuthi watu vilevile na kuwaua watu.

Wakatuma watu wa hila, wakawaambia enendeni, 'mkafanya rafiki hatta 'mmwua. Wale wakaenda wa khofu. Walipofika wakafanya urafiki. Hatta siku hiyo wakamwambia, tule kikoa, Sultani. Yeye Liongo akawajibu —

Hila kikoa halipani mkata'mno.

Maana yake — Nikila kikoa nitalipa nini, masikini'mno? Wakamwambia, tule kikoa cha makoma. Akawauliza, tutakulaje? Wakamwambia, atapanda mtu 'mmoja ju ya mkoma akaangue, tule, tukiisha apande mgine, hatta tuishe. Akawaambia, vema.

Akapanda wa kwanza, wakala. Akapanda wa pili, wakala. Akapanda wa tatu, wakala. Na wale wamefanya hila, atakapopanda Liongo tu'm-

nige kwa mishare kulekule ju.

Liongo akatambua kwa akili yake. Hatta walipokwisha wote wakamwambia, haya, zamu yako. Akawaambia, vema. Akashika mkononi uta wae na viembe, akawaambia —

Tafuma wivu la angania. tule cha yayi.

Maana yake, Nitapiga bivu la ju, tnle cha kati. Akapiga, likakatika tawi, akapiga tena, likakatika la pili, akaupukusa mkoma mzima, yakajaa tele chini. Wakala. Hatta walipokwisha, wale watu wakasema wao kwa wao, ametambua huyu. sasa tufanyeje? Wakanena, twendeni zetu. Wale wakamwaga, wakamwambia —

Kukuingia hadaani Liongo fumo si mtu,
Yunga jini Liongo okoka.

Maana yake, Hukuingia ujingani Liongo mfalme, wewe si mtu, kama Sheitani umeokoka.

Wakaenda zao, wakajibu kwa yule mkuu wao, alioko mjini, wakamwambia, hatukuweza.

Wakafanya mashauri — nani atakayeweza ku'mua? Wakanena, labuda mtoto wa nduguye. Wakaenda wakamwita. Akaja. Wakamwambia, enenda, kamwuliza babayo, kitu gani kinachomwua, ukiisha ku jua, uje utwambie. na akiisha kufa tutakupa ufaume. Akawajibu, vema.

Akaenda. Alipofika aka'mkaribisha, akamw-

ambia, umekuja fanya nini? Akamwambia, nimekuja kukutazama. Akamwambia, najua mimi umekuja kuniua, na hao wamekudanganya.

Akamwuliza baba, kitu gani kinachokuua? Akamwambia, sindano ya shaba, mtu akinichoma ya kitovu, hufa.

Akaenda zake mjini, akawajibu, akawaambia sindano ya shaba ndio itakayo'mua. Waka'mpa sindano. akarudi hatta kwa babaye. Alipomwona, akaimba yule babaye, akamwambia —

Mimi muyi ndimi mwe mao. situe
Si mbwenge mimi muye ndimi mwe mao.

Maana yake, Mimi mbaya ndiye mwema wako, sinifanya mbaya, mimi ndimi mbaya ndiye mwema wako. Aka'mkaribisha, akajua, huyu amekuja, kuniua.

Akakaa siku mbili, hatta siku hiyo, usiku amelala, aka'mchoma sindano ya kitovu. Akaa'mka kwa uchungu wake, alishika uta wake na viembe, akaenda hatta karibia visima. Akapiga magote, akajitega na uta wake. Akafa palepale.

Hatta assubui, watu wanaokuja teka maji wawakamwona. waka'mthani mzima, wakarudi mbio. Wakatoa khabari mjini, leo maji hayapatikani. Kulla endaye hurudi mbio. Wakatoka watu wengi wakaenda, wakifika, walipomwona wasiwezo

ku karibia. wakarudi. Siku tatu watu wanathii kwa maji, kuyakosa.

Wakamwita mamaye, wakamwambia, enenda kasema naye mwanao, aondoke, tupate maji, ao tutakuua wewe.

Akaenda, hatta alipofika aka'mshika mwanaye ku 'mtumbuiza kwa nyimbo, akaanguka. Mamaye akalia, akajua mwanawe amekufa.

Akaenda ku waambia watu mjini, ya kwamba amekufa, wakaenda ku'mtezama, wakamwona amekufa. waka'mzika, na kaburi lake laonekana katika Ozi hatta leo.

Waka'mkamata kile kijana, waka'mua, wasi'mpe ufaume.

## MIFANO.

Haraka haraka haina baraka.

Mvunda 'nti mwana 'nti.

Ulimi hauna mfupa.

## UZA GHALI, SI UZA RAKHISI.

ALIONDOKA tajiri mkubwa mwenyi mali mengi, naye waziri wa Sultani. Akakaa katika ulimwengu wake, akazaa kijana kimoja. Na kijana kile, jinalake Ali. Hatta mtoto alipopata mwaka wa khamsi u asherini, babaye akafa. Akasalia yeye na mamaye.

Akarithi mali yake Ali, akatumia mali sana. Hatta Ali akafilisika, akawa maskini thaliththi, pasiwe mtu 'mmoja a'mjuaye katika mji ule, rafiki zake yeye, wala wa babaye. Akawa mtu kijana, akatembea katika mji.

Killa amwonaye Ali humwuliza, mali yako waliyatendani, Ali, hatta ukafilisika upesi? Kwani babayo aliacha mali mengi, ungekuwa na akili Ali, mali yako ungedumu nayo. Ali akanena, asiojua maana, haambiwi maana.

Ikawa kazi, neno lake, killa amwulizao humwambia — asiyojua maana, haambiwi maana. Hatta yale maneno mji mzima watu wamejua, kamma Ali, akimwuliza — mali yako umeyatendani, hukujibu, asiyojua maana, haambiwi maana.

Hatta maneno yakafika kwa Sultani. Watu wakamwambia Sultani, yule kijana wa waziri wako, Ali, amefilisika, watu wakimwuliza — mali yako, Ali, waliyatendani hatta yakaisha upesi? Mali yako ni mengi aliokuachia marehemu babayo, kwani mali yake, ungekuwa na akili, Ali, yangedumu nawe, kwa yale mali kwa kuwa mengi. Na Ali hujibu, akamwambia amwulizaye — asiojua maana, haambiwi maana.

Sultani akanena, kaniitieni Ali, aje ni'mulize maneno haya kweli wanaonena watu ao wana'msingizia. Akaondoka Kathi akanena, naam, kweli, Sultani, maneno haya. Akatuma asikari kwenda kumwita kuja wakati wa baraza, na watu pia walipo katika baraza ya Sultani waje, wasikie, maneno haya anaonena Ali kweli ao uwongo.

Hatta Ali akaenda akaazima kanzu mbovumbovu kwa mtu maskini, kwani hapana mtu anayomwamini ku 'mpa nguo zake, na hiyo kanzu Ali apata kwa tafáthali na kwa angukia.

Hatta akaenda mwangoni mwa Sultani, na baraza imejaa tele watu, na Sultani amekaa kitako. Sultani akaondoka, akamwita — Ali! Akaitika — Lebeka. Akamwambia, Ali, nimesikia maneno kama mali yako yamefilisika, na wewe huwajibu watu wanayokuuliza, huwaambia — Asiyo-

jua maana, haambiwi maana.

Akamwambia — Na'am Bwana, mali haya naliyapiga mafungu manne, fungu moja nalitia baharini, fungu moja nalipiga moto, fungu moja nalikopesha wala sitalipwa, fungu moja nimelipa deni wala sijaisha kulipa.

Sultani akamwambia — Ali, uza ghali siuza rakhisi. Ali akamwambia — Ee Walla, hababi. Akatoka, akaenda zake.

Akaondoka waziri wake Sultani palepale, katika baraza, akamwambia — Seyedina, maneno haya nayajua maana yake. Sultani aka'mjibu, akamwambia, kamma wee uyajuapo maneno haya maana zake, billa ku mwuliza Ali, uyajue kwa akili yako, mimi Sultani ntakupa usultani wangu, kinachosema na kisichosema katika milki yangu. Mimi Sultani nimekupa, yako. Na wewe usipojua maneno haya maana zake kwa akili yako, mali yako nitatwaa yote, wallakini usimwulize Ali.

Akanena waziri, nisipojua maneno haya kwa akili zangu, mimi waziri katika milki yangu nimekupa, Sultani, kinenacho na kisichonena, illa mke wangu mtoto wa watu enda kwao, na kitwa changu halali yako, Sultani.

Sultani akanena, na mimi ntashuka katika u-

faume niwe ndiye waziri wako, mimi Sultani.

Akaondoka waziri, akaenda hatta nyumba yake, akanama, akafikiri, akaenda akatwaa vyuo viliomo jamii ndani ya nyumba yake. Akavifunua ku tazama maana ya maneno ya Ali, asipate kimoja kilichomo maneno ya Ali. Bassi akakaa kitako akifikiri na ku aza — mimi nimenena kwa Sultani, maneno haya ntayajua kwa akili zangu, nami nimetafakari na ku waza sikuyajua.

Akamwita Juma — Yule kijana Ali anakaa wapi? Akamwambia — Bwana, Ali gani?

Akamwambia. Kule kijana aliokuwa na mali mengi, kijana cha waziri marehemu Hassan, aliofilisika, hu'mjui anakokaa? .Tafáthali unipeleke nna maneno naye ku taka ku mwuliza. Na maneno haya nimekwambia wewe, usimwambie mtu tena. Nami nimekuacha huru kwa sababu maneno haya asijue 'mtu.

Akamwambia — Ee Walla! Ee Walla! na'mjua anakokaa. Kule-e-e mwisho wa mji, kuna kipenu kidogo karibu na pwani, ndiko anakokaa kwa yule masikini mwenyi chongo anayopita akiomba, ndiye rafiki yake, ndiko anakokaa, hana pahali pangine.

Akaondoka waziri usiku, saa ya sita, watu pia wamelala, yeye na mtumwa wake 'mmoja, huyu

mtumwa ndiye msiri wake, wakaenenda hatta wakafika. Akabisha yule waziri katika kile kipenu, akamwita — Ali! Ali! Akaogopa, asiitike. Akamwambia — Ali!

Akamwambia rafiki yake, a'mka, a'mka. Akamwuliza, kuna nini? Akamwambia, kumepiga mtu kibandani kwetu, nami nataajabu usiku huu, huyu mtu mlevi, ao mtu atakayokuja kwiba uko ndani? Lakini sisi fukara, hatuna kitu. Labuda mtu ataka ku tuhusudu, ku tutoa roho zetu. Akamwambia, lakini mimi, na tukae kitako kwanza tusikilize, hatta atakapobisha mwango huu marra ya tatu tumwitikie, hwenda tuka'mjua sauti yake.

Akamwambia, gissi gani wewe, Ali, kuwa mjinga? Mtu amekuja usiku wa manane, hatu'mjui atokako, na sisi hatuna kawaida ya kuja mtu ku bisha mwango kwetu, ataka nini mtu huyu, isipokuwa labuda ana mambo matatu ataka kwetu, kama Muungu amenijalia mambo haya nayawaza mimi katika roho yangu, ni lile apendalo Mwenyi ezi Muungu.

Akamwambia Ali — Gissi gani, rafiki yangu, maana ya tatu gani haya, unayowaza wewe katika roho yako? Nambie nami najue, tupate ku jua sote. Nambia la kwanza.

Akamwambia, la kwanza, ataka kuja kwiba;

la pili, ataka kuja ku tuua; la tatu, labuda anasema huku kuna 'mke wake, ao mtumwa wake mwana'mke. Ndiyo ninayoyawaza mimi katika roho yangu.

Akamwambia, sijui, rafiki yangu, linalokuja kwa Muungu lote jema.

Ali akasema, akibisha sasa nitamwitikia, akiniua na aniue, akiniacha — bass, wala sina buddi illa ku mwitikia.

Akabisha waziri, akamwita — Ali! Akamwitikia, lebeka,. nani weye unayokuja niita usiku, na usiku huu umekuwa wa manane? Akamwambia, ni mimi. nina shughuli nawe. Akamwambia, sikujui weye. bwana, uliokuja. Akamwambia, usiogope, nimekuja kwita kwa kheri, sikuja kwita kwa shari. Akamwambia, bwana, kuniita kwako, ndiko unisaburi hatta assubui. Waziri akamwambia, hapa nilipo, siwezi kukusaburi hatta kwa dakika moja, hivyo unavyonena ndani naona unakawia. Tafăthali, Ali, toka nje, usikie nenò langu nalikwitia.

Akamwambia — Ee Walla, bwana, naweka sikio langu katika mwango uniambie jina lako, ndiyo nitakapoamini ku toka kwani ndipo nimekwisha ku kujua.

Akaenda waziri akamwambia, ni mimi, Wa-

ziri wa Sultani, tafáthali toka. 'una maneno nawe kwambia na maneno haya kwa faragha. Ee Walla, bwana wangu. Akaenda Ali akamwambia rafiki yake, yule maskini, nimekuja kwitwa na waziri wa Sulṭani, hukatai witwa hukataa aitiwalo.

Akamwambia, rafiki yangu enenda, labuda kuna kheri nawe. Akifungua mwango, Ali akimwona waziri na mtumwa wake 'mmoja. Akamwambia, Bwana, masalkheiri. Akamwambia, marahaba, Ali, tuondoke, twende zetu kwangu. Akamwambia — Ee Walla, Bwana.

Yule waziri na Ali wakafuatana hatta nyumbani kwake. Waziri akipanda darini, saa saba ikipiga ya usiku. Waziri akamwita mjakazi wake — Mrashi! Akaitika — lebeka. Kamwambie bibi afanye chakula kwa upesi, kabla saa ya nane hajapiga, na wewe regea.

Alipokuja Mrashi, akamwambia — nimekuja, Bwana. Akamwambia, Mrashi, ukafungue kasha, lete kitambi kimoja cha kilemba, ulete na kofia moja nyeupe ya darizi, lete na kanzu moja ya khuzurungi, ulete na kikoi kimoja seyedia ya uzi, na zote nimefunga pamoja katika bahasha ya leso nyekundu, upesi ulete.

Akaondoka waziri akamwambia Ali, nimekwitia kheri, tafáthali maneno yangu haya asijue

mtu, weka ndani nafsi yako. Ali akamwambia, Ee Walla, Bwana, mimi maneno yako nayaweza kuyatoa, Bwana?

Akamwambia, nataka, Ali, unipe maana ya maneno yale waliyomwambia Sultani, unipe na maneno aliokujibu Sultani.

Akamwambia, Sultani ameniambia — Uza ghali, si uza rakhisi.

Ali, Ali, utafáthali ukanambie maneno haya, utanambiaje, na Sultani ameniambia, uza ghali, si uza rakhisi? Ntakupa shamba langu.

Akamwambia, Sultani ameniambia, uza ghali si uza rakhisi.

Akamwambia, Ali, bokhari zangu zote twaa zilio mjini.

Ali akanena, Sultani ameniambia, uza ghali si uza rakhisi.

Waziri akanena, Ali, twaa yote mashamba yangu.

Ali akanena, Sultani ameniambia, uza ghali si uza rakhisi.

Waziri akamwambia, twaa yote milki yangu.

Ali akanena, Sultani ameniambia, uza ghali si uza rakhisi.

Waziri akamwambia, twaa kisemacho na kisichosema katika milki yangu mimi waziri, nami

nambie maneno haya.

Ali akanena, Sultani ameniambia, uza ghali si uza rakhisi.

Akaondoka waziri, akamwambia, ntakupa nyumba yangu yote 'nnaokaa na mali yaliomo yote, illa 'mke mwana watu enda kwao.

Akamwambia, bassi sasa niandikie khati ya mkono wako.

Waziri akamwita Mrashi. Akamwitikia, lebeka, Bwana. Akamwambia, lete kalamu na wino na karatasi kishubakani. Mrashi akaenda akaleta. Waziri akakamata karatasi na wino, akamwandikia Ali, nime'mpa yote milki yangu kinenacho na kisichonena, hatta nyumba yangu nikaao mwenyewe, illa 'mke mwana wa watu enda kwao. Akatwaa khati waziri aka'mpa Ali.

Imekuwa saa ya kumi, tuondoke tukasali kwanza, ku regea kwetu ku sali nikupe maana zako unazozitaka.

Wakashuka wakaenda zao ku sali, wakarudi mosketini. Akamwambia, — haya, Ali, nambie, kwani tena kumekucha.

Ali akamwambia, maana ya ku nena "asiojua maana haambiwi maana," kwa sababu nikimweleza mtu asiokuwa na akili hatajua. Ndio maana killa aniulizaye nikimwambia — asiojua maa-

na haambiwi maana. Na Sultani aliponiita akaniuliza hayaambiwi, kwani Sultani ana akili. Naye, ndiyo akanijibu — Uza ghali, si uza rakhisi. Haya maneno yako.

Bassi nieleze mali haya yalipotea.

Ali akanena, mali haya naliyapiga mafungu manne, fungu moja nalitia baharini, fungu moja nalipiga moto, fungu moja nalikopesha wala sitalipwa, fungu moja nimelipa deni wala sijaisha ku lipa.

Bassi, nambie, Ali, maana ya ku tosa baharini fungu moja, maana yake nini?

Ali akamwambia waziri, niwie rathi kwa killa nitakalonena stahamili. Akamwambia, baharini ni mali naliyokwenda ku fanya usherati na waanaake, yamepotea mali yale sitayapata tena, bassi kama naliyotia baharini, kwani kitu kikizama bahari hakipatikani.

Na maana ya ku piga moto fungu moja?

Ali akanena, nalikula sana, nalivaa sana, nalitumia sana, ndiyo maana ya ku piga moto, kwani havitaregea tena katika mikono yangu.

Nambie fungu la tatu, maana ya ku kopeshwa wala hutalipwa nini?

Akamwambia waziri, ni kama mtu walio'mpa mkeo mahari yake, haitarudi tena, bassi ndio

maana ya ku kwambia nimekopesha wala sitalipwa.

Akamwambia, fungu la 'nne nambie maana yake ya ku nena umelipa deni wala hujaisha ku lipa.

Akamwambia waziri, ni kama mtu alio'mpa mama yake mali ku taka ku 'mfurahisha roho yake, walakini mimi mtoto sijui kama mama yangu ni furahi roho yake kwa haya naliyo'mtendea, bassi na mimi kijana hunena rohoni mwangu, hajaisha mama yangu ku furahi kwa yale nalio'mpa mali. Ndio maana ya ku kwambia, nimelipa wala sijaisha ku lipa.

Akamwambia, ahsánt, Ali, na maneno yako nimeyasikia.

Nao kumekuwa jua la chomoza, saa kumi na mbili zimekwisha piga. Akakaa waziri na roho yake furaha — nitakwenda leo ku pata usultani, kwani nimeyajua kwa akili yangu. Akakaa waziri hatta saa ya tatu Sultani amebarizi. Akitoka nyumbani mwake waziri hana kitu illa kanzu yake moja ilio mwilini mwake. Akatoka na furaha roho yake.

Akaenda hatta akafika mbele ya mwángo wa Sultani. Watu waliopo na asikari jamii waliopo wakastaajabu — Ah! Waziri mkubwa, ndiye

mweyi mambo yote ya Sultani, anakuja kwa kanzu moja, hatta viatu miguuni hana. Hatta watu wana'mtaajabu pasiwe mtu 'mmoja aliojua alionalo katika roho yake. Wale watu wajinga wakanena, labuda anafiwa na mkewe. Ndiye akaja vile kwa Sultani.

Akaondoka waziri, akamwambia — Subulkheiri Seyedina. Sultani akamwambia — Allah bilkheir al wazir, karib. Akakaa kitako.

Snltani akanena; nambie khabari zako, walizonazo. Akamwambia, khabari kheri, nimekuja kukupa maana ya maneno yako yale twalioahadiana mimi nawe, Sultani. Nami nimeyajua kwa akili zangu, Sultani.

Sultani akamwambia, nieleze la kwanza.

Akamwambia, yule Ali walipo watu waka'muliza, kwani mali yake yakafilisika, kuwaambia, asiojua maana haambiwi maana, kwa sababu wale watu wajinga hatawaambia maneno yale. Hawajui la ku 'mjibu, bassi si afathali hawaambii wasiojua maana? Kwani mwenyi ku mwambia mtu neno ataka ku jibiwa. Utamwambia mtu neno hajui la ku jibu? Bassi ndio maana yake asiawambie. Sultani akanena, na'am, inna kweli maneno haya. Akamwambia, nipe maana, waziri, ya mafungu manne haya.

Akamwambia, la kwanza, Sultani, lilitoswa baharini fungu moja, na moja lalipigwa moto, na moja lalikopeshwa wala hatalipwa, na moja amelipa wala hajaisha ku lipa. Akamwambia, na'am waziri, inna maneno yako kweli.

Akamwambia, nipe maana ya ku toswa baharini fungu moja hili. Akamwambia, ni mali aliotwaa Ali akaenda ku fanya usherati nje, mali yale yakapotea, ndiyo maana ya ku ambiwa, fungu moja lile limeingia baharini.

Akamwambia, na'am waziri, inna neno hili kweli. Sultani akanena, hii fetha kwisha ku peleka waanawake fetha haipatikani tena, kweli maneno yake, kama imeingia baharini. Nipe na maana ya fungu la pili liliopigwa moto, nipe maana yake.

Akanena waziri, Ali alikula sana, alivaa sana, alitumia sana, ndiyo maana ya ku pigwa moto mali zile, hazitaregea tena mkononi mwake.

Sultani akanena, na'am inna kweli maneno haya, waziri, kwani hii mali ukiisha ku nunua chakula, ukanunua na nguo njema, ukavaa, imekwisha potea mali hairudi. Maneno yake amenena kweli Ali, kama fungu hili limepigwa moto. Akamwambia, nambie, waziri, katika fungu la tatu maana yake.

Waziri akanena, fungu la tatu amelikopesha, wala hatalipwa. Akamwambia, maana yake nini ya ku kopesha mali hayo wala hatalipwa? Waziri akanena, ni mali aliyetoa ku 'mpelekea mahari yake mana'mke, utapomwacha, mali yako hakurudishii, ndio maana, akanena, nimekopesha sitalipwa.

Akamwambia, na'am waziri, inna maneno haya kweli. Sultani akanena, mwenyi ku'mpa mana'mke mahari hapati tena, utakapokuwa manamume amefilisika, hafanyi roho yake njema yule mana'mke ku kupa. Kwani umekuwa masikini, akuona kama mjinga, hakujui kama aliokuwa mume wangu, kwani umekuwa fukara, tena umekuwa mbaya, tena amekufanya mtu mjinga, kwani umekosa mali. Kwani walipokuwa na mali walikuwa manamume mzuri, walikuwa kijana una akili, walionekana kama kijana cha Sultani.

Akaondoka waziri akanena, kweli, Sultani, mtu akikosa mali hawi mtu mbele za watu. Sultani akanena — Waziri, nambie maana ya fungu la 'nne, ku lipa wala hajaisha ku lipa.

Akamwambia Sultani, maana yake, Ali alitoa mali katika fungu moja aka'mpa mamaye. Bassi Ali hajui kama mamaye roho yake i rathi kwa mali aliyopewa na mwanawe. Bassi Ali ananena,

labuda mama yangu hajafurahi kwa lile nalilo'mtendea, ndio maana ya ku nena Ali, ku lipa wala sijaisha ku lipa.

Sultani akamwambia, na'am waziri. Akaondoka kitini akasimama, na baraza imejaa tele watu, akamwita akida, akamwambia, nenda gerezani kamwamuru jemadari apige goma, sasa amekuwa Sultani waziri wangu, na mimi ndiye nimekuwa waziri wake; na ninyi jamii asikari, na jamii ya walio 'mliomo katika mji, Waarabu, na Waswahili, na jamii Wangazidja, 'mtiini Sultani.

Akiondoka, akautwaa usultani waziri.

Bass, wakakaa kitako mda wa siku mbili.

Mtu akipita kwa nyumba iliokuwa wa waziri a'mkuta Ali katika dirisha, anachungulia anamwa'mru mchunga ku tandika frasi, ataka kwenda ku tembea. Yule Mwarabu akamwita — Ali! akamwitikia — na'am. Mbona u katika nyumba hii? Ali akamwambia, Sultani hakuniambia, uza ghali si uza rakhisi, ati? Nami nimekuza ghali.

Ahh! Yule Mwarabu akataajabu — gissi gani huyu Ali kuwa katika nyumba ya waziri mkubwa — lakini haithuru. Akakaa.

Akapita Mwarabu mgine aka'mkuta chini sebulani, akamwita — Ali! Akamwitikia — naam. Akamwambia, mbona nakuona hapa, Ali? Aka-

mwambia, hii si nyumba yangu? Gissi gani kuwa hii nyumba yako? Sultani ameniambia, uza ghali si uza rakhisi, nami nimekuza ghali ati.

Akaondoka yule Mwarabu, akaenenda hatta mwangoni kwa Sultani. Akamwambia, bwana wangu, seyedi yangu, nimekuta mtumwa wako, Ali, katika nyumba ya waziri wako, nikamwuliza — Ali? Akaitika, na'am. Unafanyaje katika nyumba hii wewe? Ali akanijibu, Sultani ameniambia, uza ghali si uza rakhisi, nami nimekuza ghali.

Yule Sultani akataajabu — ndio mambo alionitenda waziri, nami naye twalipana wahadi wa ku tosha ku mwuliza Ali, kumbe yeye amekwenda ku mwuliza Ali, na mali yake ku filisika? Bassi sasa mbona amekosa kuwili, amekosa mali yake amekosa na usultani. Na weye upesi enenda kamwita Ali aje. Ee Walla, Bwana.

Akitoka mbio kwenenda aka'mkuta Ali, ataka ku ingia mashuani kwenda ku tembea. Akamwita, Ali! Akamwambia, na'am. Akamwambia upesi, unakwitwa kwa Sultani. Ali akanena, Ee Walla, ni kama Sultani, Sultani wangu.

Akaondoka Ali akapanda darini, akamwita — Mrashi, nitezamie katika nguo njema ziliomo katika makasha, kwani wewe ndiye ujuaye zayidi

kuliko mgine. Akaenda Mrashi akifungua kasha akitoa joho mzuri, akatoa kilemba kizuri, akatoa na deuli aali, akatoa na janvia moja la temsi la thahabu, akatoa na kitara kimoja cha albunsayidi cha Arabu, akatoa na kitupa cha hal wáradi Stambuli, aka'mpelekea bwana.

Alipoziona Ali nguo zile akafurahi, akatwaa, akavaa, akishuka na yule Mwarabu, wakaenenda hatta wakafika katika mwango wa Sultani. Wakamwambia, pita sebulani. Akapita, akakaa kitako.

Akishuka yule Sultani kuja chini ku barizi, akashuka na yule aliokuwa Sultani kwanza, sasa aliokuwa waziri. Akamwambia waziri, akaitika, na'am. Akamwuliza, zile sharti zetu hazikufaa, nalikwambia mimi sharti zangu ujue kwa akili yako usiende ku mwuliza Ali? Akamwambia, naam. Na wewe ukazunguka, ukaenda ku mwuliza Ali. Akamwambia Sultani, sikumwuliza Ali. Sultani akanena, Ah! Ali si huyu yuko? Akamwambia, tumwite, aje mbele zako tupate ku sadiki kama maneno haya kuyajua kwa akili yako wewe, ila kwa Ali kukwambia. Akamwambia, na'am, mwita Ali aje.

Akaondoka Sultani, akamwita Ali. Akamwambia, lebeka, hababi. Akamwambia, njoo. A-

kamwambia, gissi gani wewe, Ali, kwenda ku kaa katika nyumba ya waziri, una maana gani? Akamwambia, na'am, Sultani, waliniambia wewe, uza ghali si uza rakhisi, na khati ya waziri hii alioniandikia, nawe soma, Sultani, ujue mambo haya kweli.

Sultani akaishika akaisoma khati, akamwambia, kweli, Ali, umekuza ghali hukuza rakhisi.

Akaondoka Sultani akamwita waziri. Akamwambia, lebeka hababi. Akawaambia watu, 'mlioko katika baraza, mkubwa na mdogo, na Banyani, na Mwarabu, na Msheheri, na Mngazidja, na Mswahili, na jamii ya watu waliomo katika inchi — bassi mimi nimemwondoa, hamo katika uwaziri wala katika usultani, hali yake kama hali ya waliyo katika mji. Na sasa huyu Ali ndiye amekuwa waziri wangu mkubwa, killa mtu atakalo, akiwa mume, akiwa 'mke, akiwa Mwarabu, akiwa Mzungu, wote na waende kwa Ali ndio atakokwisha mambo yenu.

Na hii hadithi imetokana na Ninga.

Mwisho.

# APPENDIX.

## A TRANSLATION

of the Verses at pp. 45-8 into the current

language of Zanzibar.

NIPENI kiti, nikae kitako,
Nipembeze Mananazi wangu,
Nipembeze mwanamke wangu,
Aniondoa hamu na simanzi.
Husimama chini ya mlango
Nikitoka kwenda ku tembea,
Nikitoka ku fanya shughuli,
Huwaambia watumishi wake,
Akamwambia Sada na Rehema
Pikeni 'msikawilie,
Pikeni, 'mfanya upesi,
'Mpike wali na mchuzi.
Akiniona nimekawilia,
Hu'mtuma kijakazi chake,
'Mtezame njia ya Sultani,
Ao kwao wa mfalme aliyetawala,

'Mtezame vikaoni vya nduguze,
Ao kwao kwa mamaye, shangazi lake,
Ka'mshike, upesi uje naye,
Wafanya nini hatta wakati huu,
Kamwambia, Bwana, unakwitwa,
Twende upesi, sifanye uvivu,
Ku kawilia kwako huchoka ku simama
Na machoni yatoka machozi.
Kamwambia twende tangulia, 'nnakuja,
Ka'mtulize, awache majonzi,
Kamfuata nyuma kwa tambo,
Akinuka mesiki na ambari.
Akipita akamwamkia,
Ka'mjibu mtoto wa Hejazi.
Marra hiyo akaondoka akasimama.
Akamweka mkono wa bega,
Kamwombea Muungu Jabari,
Ewe mama, Muungu atakujalia.
Akainua mkono Mwana
Akaupeleka ju ya mwanzi.
Akaangua kisuto cha kikale,
Kizuri kimetariziwa,
Akamweka kitulizo cha macho.
Mwana wa ndugu wa babaye, na mwana wa shangazi.
Akamwambia, Bwana tukae kitako,

Usisimame 'mno, ukafanye uvivu.
Mwiteni huyo Time aje,
Upesi, awache usingizi,
Apakue pilao ya kihindi,
Ya zabibu haina mchuzi.
Lete kiti kizuri cha Ulaya,
Na sinia njema ya Shirazi
Imetiwa nakishi,
Na sahani inang'ara kama mwezi.
Akanena watumwa na waje,
Kwa nini hamwimbi?
Marra hiyo akamwandikiwa
Na Time ameshika guduwia,
Imetiwa maji ya zabibu
Akimnywesha kama 'mnyua tembo.
Akimlisha aki'mrai
Akimwonyesha kwema malazi.
Akimlisha tambuu ya Siyu,
Laini laini ya Ozi,
Akaikunja aki'mtia kinwani,
Na iliki pamoja na lozi.
Nimekoma ku sifu mwana'mke
Wa ku chagua wangu Mananazi.

‡

MAMA, nipeleke, hatazame
Uzuri na pambo Ungama,
Hatazame mnara umepambwa,
Uliotengenezwa kwa heshima.
Na waliopamba watoto,
Wamevaa timbi na vidani,
Wamevaa sarufu na vilemba,
Na tamvua mbele va nyuma.
Wamevaa nguo za ku chagua,
Kwa watumwa mbele na nyuma.
Wamechukua panga na ngao.
Mtu hutaajabu akiona.
Amekuja Mngazidja na kopo,
Amekuja ku taka vita.
Amekuja Mgala na uta,
Amekuja ku taka ku pigana.
Tutawajengea ukuta,
Wasituingilie mjini.

* * *
* *
*